**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

# HOTUBA YA WAZIRI WA FEDHA NA UCHUMI MHE. MUSTAFA HAIDI MKULO (MB) AKIWASILISHA BUNGENI TAARIFA YA HALI YA UCHUMI WA TAIFA KWA MWAKA 2008 NA MALENGO KATIKA KIPINDI CHA MUDA WA KATI (2009/10-2011/12)

## UTANGULIZI

1. **Mheshimiwa Spika,** naomba kutoa hoja kwamba Bunge lako Tukufu sasa likae kama Kamati ili liweze kupokea na kujadili Taarifa ya Hali ya Uchumi wa Taifa katika kipindi cha mwaka 2008 na malengo katika kipindi cha Muda wa Kati (2009/10 – 2011/12). Pamoja na hotuba hii, nawasilisha Kitabu cha Hali ya Uchumi wa Taifa katika mwaka 2008; na Kitabu cha Mpango wa Maendeleo wa mwaka 2009/10.

2. **Mheshimiwa Spika,** awali ya yote napenda kutoa shukrani zangu za dhati kwa Kamati ya Bunge ya Fedha na Uchumi ikiongozwa na Mwenyekiti wake Mhe. Dkt. Abdallah Omari Kigoda Mbunge wa Handeni kwa kutupatia

ushauri na maelekezo wakati wa kujadili muhtasari wa taarifa hii. Mchango wa Kamati hii siku zote umekuwa na umuhimu wa pekee katika kuboresha taarifa ya hali ya uchumi na mapendekezo ya mwelekeo wa bajeti inayowasilishwa katika Bunge lako tukufu kila mwaka.

3. **Mheshimiwa Spika,** nachukua nafasi hii pia kuwapongeza, Wabunge wapya waliochaguliwa katika kipindi cha mwaka mmoja uliopita tangu Bajeti ya mwaka jana. Napenda kuwapongeza Mhe. Charles Mwera, Mbunge wa Jimbo la Tarime, Mhe. Mchungaji Luckson Mwanjale Mbunge wa Jimbo la Mbeya Vijijini na Mhe Lolensia Bukwimba Mbunge wa Jimbo la Busanda kwa kushinda chaguzi ndogo zilizofanyika katika kipindi hicho.

4. **Mheshimiwa Spika,** kwa masikitiko makubwa, napenda kutoa pole kwa ndugu, jamaa na familia za Waheshimiwa Wabunge wenzetu waliofariki katika kipindi hiki cha mwaka mmoja. Hayati Chacha Zakayo Wangwe aliyekuwa Mbunge wa Tarime, Hayati Richard Nyaulawa aliyekuwa Mbunge wa Mbeya Vijijini, Hayati Faustine Kabuzi Rwilomba aliyekuwa Mbunge wa Busanda, na Hayati Phares Kabuye ambaye alifariki kabla ya shauri la pingamizi la kutengua ubunge wake wa jimbo la Biharamulo Magharibi kukamilika. Tunamwomba Mwenyezi Mungu aziweke roho za marehemu mahali pema peponi. Amina.

5. **Mheshimiwa Spika,** baada ya kusema hayo, sasa naomba nianze kutoa muhtasari wa mapitio ya hali ya uchumi na maendeleo kwa mwaka 2008 ikiwa ni mapitio ya mwaka wa nne wa utekelezaji wa Mkakati wa Kukuza Uchumi na Kupunguza Umaskini Tanzania (MKUKUTA). Kwa kipindi cha mwaka 2008/09, bajeti iliendelea kujikita zaidi katika kuendeleza mageuzi ya kiuchumi na kijamii yaliyolenga katika kukuza na kutengemaza uchumi kwa kutekeleza sera, mipango, programu na mikakati mbalimbali ya kuharakisha maendeleo ya kiuchumi na kijamii ya Taifa letu. Aidha, ikumbukwe kwamba taarifa hii ni ya kipindi cha kuanzia Januari hadi Desemba 2008 na sehemu chache zimegusia robo ya kwanza ya mwaka 2009.

## MAPITIO YA MWENENDO WA UCHUMI JUMLA KATIKA KIPINDI CHA MWAKA 2008

6. **Mheshimiwa Spika,** mwaka 2008 ulikuwa mwaka ambao Dunia ilikumbwa na matatizo makubwa ya kiuchumi na kijamii. Katika mwaka huo, masoko ya fedha na mitaji yalikumbwa na misukosuko hasa katika nchi zilizoendelea hususan Marekani na nchi za Ulaya. Aidha, tulishuhudia kupanda kwa bei ya mafuta katika soko la dunia kufikia kiwango cha juu

zaidi ambacho hakijawahi kutokea, na bei za chakula kuwa za juu katika nchi mbalimbali.

**Pato la Taifa**

7. **Mheshimiwa Spika,** pamoja na kuanguka kwa uchumi wa dunia kulikosababishwa na msukosuko katika sekta ya fedha, Pato Halisi la Taifa lilikua kwa asilimia 7.4 mwaka 2008 ikilinganishwa na asilimia 7.1 mwaka 2007 . Ukuaji huu ulichangiwa zaidi na kuongezeka kwa viwango vya ukuaji katika shughuli za kiuchumi za kilimo, uvuvi na huduma. Ukuaji wa viwango vya juu ulijionesha katika shughuli ndogo za kiuchumi za mawasiliano (asilimia 20.5); fedha (asilimia 11.9); na ujenzi (asilimia 10.5). Kwa ujumla, kiwango cha ukuaji katika shughuli za kiuchumi za viwanda na ujenzi kilipungua. Mchango wa shughuli za kiuchumi za huduma umeendelea kuongezeka katika mwaka 2008 ikilinganishwa na shughuli nyingine za kiuchumi.

8. **Mheshimiwa Spika,** kutokana na kukua kwa Pato la Taifa kutoka shilingi bilioni 20,948.4 mwaka 2007 hadi shilingi bilioni 24,781.6 mwaka 2008 na idadi ya watu Tanzania Bara iliyokadiriwa kuwa watu milioni 39.5, Pato la Wastani la kila Mtanzania liliongezeka hadi shilingi 628,259 mwaka

2008 ikilinganishwa na shilingi 548,388 mwaka 2007, sawa na ongezeko la asilimia 14.8.  Pato hili la wastani ni sawa na dola za Kimarekani 525.1.

**Kasi ya Upandaji Bei**

9. **Mheshimiwa Spika,** wastani wa kasi ya upandaji bei kwa mwaka 2008 ulikuwa asilimia 10.3 ikilinganishwa na asilimia 7.0 mwaka 2007. Kiwango cha chini cha kasi ya upandaji bei katika mwaka 2008 kilikuwa mwezi Januari ambapo kasi ya upandaji bei ilikuwa asilimia 8.6 na kiwango cha juu kilikuwa asilimia 13.5 kilichojitokeza katika mwezi wa Desemba 2008.

10. **Mheshimiwa Spika,** lengo tulilolíweka kwa ajili ya kudhibiti mfumuko wa bei lilikuwa asilimia 5.0 hadi kufikia mwezi Juni, 2008. Lengo hili halikufikiwa kutokana na kuongezeka kwa gharama za nishati, hususan ya umeme, kupanda kwa bei ya mafuta pamoja na bei ya chakula. Hadi Aprili 2009, mfumuko wa bei ulifikia asilimia 12.0. Kutokana na hali hiyo, lengo la mfumuko wa bei  ambalo awali lilikadiriwa liwe chini ya asilimia 7.5 ifikapo Juni 2009 sasa tunatarajia litafikia asilimia 11.0.  Mwezi Mei, 2009, mfumuko wa bei ulikuwa asilimia 11.3.

**Ukuzaji rasilimali**

11. **Mheshimiwa Spika,** katika mwaka 2008, ukuzaji rasilimali uliongezeka kufikia shilingi bilioni 7,381.3 kutoka shilingi bilioni 6,209.7 mwaka 2007, sawa na ongezeko la asilimia 18.9. Kuongezeka kwa ukuzaji rasilimali kulitokana hasa na kuongezeka kwa uwekezaji katika ujenzi wa majengo; uagizaji wa vifaa vya uwekezaji mitaji; na kuongezeka kwa shughuli nyinginezo za ukuzaji rasilimali zikiwemo uendelezaji ardhi, barabara na madaraja. Uwiano wa ukuzaji rasilimali na Pato la Taifa kwa bei za miaka husika ulikuwa asilimia 29.7 ikilinganishwa na asilimia 29.6 mwaka 2007.

**Ujazi wa Fedha na Karadha**

12. **Mheshimiwa Spika**, katika mwaka ulioishia Desemba 2008, ujazi wa fedha kwa tafsiri pana (M2)[1] uliongezeka kwa asilimia 29.7 ikilinganishwa na asilimia 27.0 Desemba 2007. Ujazi wa fedha kwa tafsiri pana zaidi (M3) ulikua kwa asilimia 24.0 Desemba 2008, ikilinganishwa na asilimia 21.4 Desemba 2007. Ongezeko la M2 lilichangiwa na kuongezeka kwa mikopo kwenda sekta binafsi na kuongezeka kwa amana za hundi na za muda maalum.

---

[1] *M0 ni fedha zilizo kwenye mzunguko nje ya mabenki; M1=M0 + amana za hundi; M2 = M1 + amana za muda maalum + amana za akiba; M3 = M2 + amana za fedha za kigeni (foreign deposits)*

13. **Mheshimiwa Spika,** mikopo iliyoelekezwa katika sekta binafsi iliongezeka na kufikia shillingi bilioni 4,376.4 katika mwaka ulioishia Desemba 2008 ikilinganishwa na shilingi bilioni 2,976.3 zilizotolewa Desemba mwaka 2007, sawa na ongezeko la asilima 47.0. Ukuaji huu wa mikopo unatokana na Serikali kuendelea kupunguza mikopo yake kutoka vyombo vya fedha vya ndani, kuongezeka kwa uaminifu kwa wakopaji, kuongezeka kwa dhamana ya mikopo (credit guarantee schemes), na kuongezeka kwa mikopo kwa makampuni. Sehemu kubwa ya mikopo hii ilielekezwa katika sekta za: biashara asilimia 16.1; uzalishaji bidhaa viwandani asilimia 13.1; uchukuzi na mawasiliano asilimia 8.7; kilimo asilimia 8.3; na mikopo binafsi asilimia 19.6.

14. **Mheshimiwa Spika,** wastani wa riba zilizotozwa na benki mbalimbali za biashara umeendelea kuwa na pengo kubwa kati ya riba za amana na zile za mikopo. Wastani wa riba za mikopo katika benki za biashara uliongezeka kutoka asilimia 15.25 mwezi Desemba 2007 hadi asilimia 16.05 mwezi Desemba 2008. Aidha, riba za amana za akiba ziliongezeka kutoka asilimia 2.65 mwezi Desemba 2007 hadi asilimia 2.68 mwezi Desemba 2008.

## Thamani ya Shilingi ya Tanzania

15. **Mheshimiwa Spika,** thamani ya shilingi ya Tanzania kwa dola ya Kimarekani ilikuwa ni shilingi 1,280.30 mwishoni mwa Desemba 2008 ikilinganishwa na shilingi 1,132.09 mwishoni mwa Desemba 2007. Kushuka kwa thamani ya shilingi ya Tanzania kunatokana na mahitaji makubwa ya dola za Kimarekani kwa makampuni yanayoingiza bidhaa nchini pamoja na baadhi ya makampuni kutaka kuhodhi fedha za kigeni kutokana na ubahatishaji wa kupata faida zaidi (speculation). Hata hivyo, wastani wa mwaka wa thamani ya shilingi ya Tanzania ulikuwa shilingi 1,196.3 kwa dola moja mwaka 2008 ikilinganishwa na wastani wa shilingi 1,244.1 kwa dola moja mwaka 2007.

## Akiba ya Fedha za Kigeni

16. **Mheshimiwa Spika,** mwaka 2008, akiba ya fedha za kigeni iliongezeka kwa asilimia 3.9 hadi kufikia dola milioni 2,869.7 kutoka dola milioni 2,761.9 mwaka 2007. Kiasi cha akiba ya fedha za kigeni mwaka 2008 kilikuwa kinatosheleza uagizaji wa bidhaa na huduma kwa miezi isiyopungua 4.6 ikilinganishwa na miezi 5 mwaka 2007.

**Bajeti ya Serikali**

**Mapato**

17. **Mheshimiwa Spika,** katika kipindi cha Julai 2008 hadi Machi 2009, mapato ya ndani yalifikia shilingi bilioni 3,199.1, sawa na asilimia 20.4 zaidi ya makusanyo ya kipindi kama hicho mwaka 2007/08. Hata hivyo, kiasi hiki ni asilimia 9.0 chini ya makisio ya shilingi bilioni 3,529.2 kwa kipindi hicho. Upungufu huu unatokana na kupungua kwa makusanyo ya kodi ya mapato, ushuru wa bidhaa na forodha. Tathmini iliyofanyika hivi karibuni inaonyesha kuwa hadi Juni, 2009 makusanyo ya mapato ya ndani yatakuwa chini ya lengo kwa takribani asilimia 10, sawa na pengo la shilingi bilioni 480.

**Matumizi**

18. **Mheshimiwa Spika,** katika kipindi kilichoishia Machi 2009, matumizi ya Serikali yalifikia shilingi bilioni 4,657.9 ikiwa ni asilimia 13 chini ya makisio ya matumizi. Kupungua kwa matumizi hayo kunatokana na upungufu wa makusanyo ya mapato katika kipindi hicho. Hotuba ya Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Serikali kwa mwaka 2009/10 nitakayowasilisha leo jioni itabainisha kwa kina mwenendo wa mapato na

matumizi ya Serikali kwa mwaka 2008/09 pamoja na makadirio ya mwaka 2009/10.

**Deni la Taifa**

19. **Mheshimiwa Spika,** hadi kufikia Desemba 2008, deni la Taifa lilifikia Dola za Kimarekani milioni 6,329, ikilinganishwa na Dola za Kimarekani milioni 5,891.9 Desemba 2007. Deni hilo ni sawa na asilimia 32.6 ya Pato la Taifa ikilinganishwa na asilimia 31.8 ya mwaka 2007. Kati ya kiasi hicho, Dola za Kimarekani milioni 4,822.0 ni deni la nje na Dola za Kimarekani milioni 1,507 sawa na shilingi bilioni 1,929.3 ni deni la ndani. Deni la nje limeongezeka kwa asilimia 14.3 ikilinganishwa na Dola za Kimarekani milioni 4,218.5 mwaka 2007. Ongezeko hilo limetokana na malimbikizo ya riba ya deni la nje hasa kwenye nchi zisizo wanachama wa kundi la Paris, kushuka kwa thamani ya shilingi na mikopo mipya. Deni la ndani kwa kipindi kinachoishia Desemba 2008 liliongezeka kwa kiasi cha shilingi bilioni 35 sawa na ongezeko la asilimia 1.8 ukilinganisha na kipindi kilichoishia Desemba 2007. Pamoja na kuongezeka kwa deni la Taifa, bado deni hilo linahimilika (Sustainable).

**Sekta ya Nje**

20. **Mheshimiwa Spika,** mwaka 2008, thamani ya mauzo ya bidhaa nje ya nchi ilikuwa dola za Kimarekani milioni 3,036.7 ikilinganishwa na dola milioni 2,226.6 mwaka 2007, sawa na ongezeko la asilimia 36.4. Ongezeko hilo lilichangiwa na kuongezeka kwa mauzo ya bidhaa asilia. Thamani ya mauzo ya bidhaa asilia zikiwemo pamba, chai, tumbaku, korosho, kahawa, katani, na karafuu iliongezeka hadi dola za Kimarekani milioni 418.4 mwaka 2008 ikilinganishwa na dola milioni 319.7 mwaka 2007. Thamani ya mauzo ya bidhaa zisizo asilia ilikuwa dola milioni 2,270.6 mwaka 2008, ikilinganishwa na dola milioni 1,704.5 mwaka 2007, sawa na ongezeko la asilimia 28.8. Ongezeko hili lilichangiwa zaidi na mauzo ya bidhaa za viwandani hasa bidhaa za nyuzi za pamba na katani. Thamani ya mauzo ya bidhaa za viwandani iliongezeka kwa asilimia 113.8 kutoka dola za Kimarekani milioni 309.8 mwaka 2007 hadi dola milioni 662.3 mwaka 2008. Aidha, mapato yatokanayo na biashara ya huduma ikijumuisha utalii, usafirishaji na huduma nyingine yaliongezeka hadi dola milioni 2,168.9 kutoka dola milioni 1,875.7 mwaka 2007, sawa na ongezeko la asilimia 15.6.

21. **Mheshimiwa Spika,** thamani ya uagizaji wa bidhaa kutoka nje iliongezeka hadi dola milioni 6,439.9 mwaka 2008 kutoka dola milioni 4,860.6 mwaka 2007. Ongezeko hili lilitokana na kuongezeka kwa uagizaji

wa bidhaa za kukuza mitaji kwa shughuli za kiuchumi katika uzalishaji viwandani, mawasiliano, uchukuzi, ujenzi na madini. Thamani ya uagizaji wa bidhaa za kati hasa mafuta iliongezeka kutokana na kupanda kwa bei ya mafuta katika soko la dunia hasa katika kipindi cha Januari hadi Oktoba, 2008. Hata hivyo, uagizaji wa bidhaa za matumizi ya kawaida ulipungua hususan uagizaji wa chakula ambao ulipungua kutoka dola milioni 315.4 mwaka 2007 hadi dola milioni 290.9 mwaka 2008 kutokana na kuongezeka kwa uzalishaji wa chakula nchini. Malipo ya huduma yaliongezeka hadi dola milioni 1,598.0 kutoka dola milioni 1,415.4 mwaka 2007, sawa na asilimia 12.9.

22. **Mheshimiwa Spika,** mwaka 2008, thamani ya mauzo ya bidhaa za Tanzania kwa nchi za Jumuiya ya Ulaya na Uswisi iliongezeka kwa asilimia 26.1; nchi za Jumuiya ya Afrika Mashariki asilimia 82.6; nchi za SADC asilimia 47.3; na nchi nyingine za Afrika asilimia 56.4. Thamani ya mauzo ya bidhaa kwenda nchi za China, Japan, India, Hong Kong na Umoja wa Falme za Kiarabu iliongezeka kwa asilimia 61.5 na Bara la Amerika kwa asilimia 51.1.

23. **Mheshimiwa Spika,** mwaka 2008, nakisi katika urari wa biashara nje iliongezeka hadi dola milioni 2,333.4 ikilinganishwa na dola milioni

2,041.6 mwaka 2007, sawa na ongezeko la asilimia 14.3. Nakisi hii ilichangiwa zaidi na kuongezeka kwa uagizaji wa bidhaa na huduma kutoka nje. Aidha, urari wa malipo yote ulikuwa na ziada ya dola milioni 108.8 mwaka 2008 ikilinganishwa na ziada ya dola milioni 412.6 mwaka 2007. Ziada hii, kwa kiasi kikubwa ilichangiwa na misamaha ya madeni iliyotolewa na wahisani katika kipindi hicho.

**HALI YA UCHUMI DUNIANI NA USHIRIKIANO WA KIMATAIFA**

24. **Mheshimiwa Spika,** kiwango cha ukuaji wa biashara duniani kiliendelea kushuka kutokana na mahitaji madogo ya bidhaa kwa Nchi Zilizoendelea na hivyo kusababisha kushuka kwa ukuaji wa biashara ya kimataifa. Katika mwaka 2008, Pato la dunia lilikua kwa asilimia 3.9 ikilinganishwa na asilimia 5.0 mwaka 2007. Kupungua kwa Pato la dunia kulitokana hasa na kuendelea kuporomoka kwa uzalishaji katika Nchi Zilizoendelea kiuchumi hususan Marekani kulikosababishwa na kuporomoka kwa soko la fedha na mitaji.

25. **Mheshimiwa Spika,** Pato la Nchi Zilizoendelea lilikua kwa asilimia 1.5 mwaka 2008 ikilinganishwa na asilimia 2.7 mwaka 2007. Kushuka kwa ukuaji wa Pato la Nchi Zilizoendelea kulitokana na kupanda kwa bei za mafuta na kupungua mauzo nje. Kwa upande wa Nchi Zinazoendelea na

Nchi za Asia zinazoinukia kiviwanda, wastani wa Pato ulipungua hadi asilimia 6.9 na 8.4 mwaka 2008 ikilinganishwa na asilimia 7.9 na 9.7 mwaka 2007 kwa mtiririko huo.

**Hali ya Uchumi wa Bara la Afrika**

26. **Mheshimiwa Spika,** kiwango cha ukuaji wa Pato la Bara la Afrika kilipungua hadi wastani wa asilimia 5.9 mwaka 2008 ikilinganishwa na asilimia 6.2 mwaka 2007. Kupanda kwa bei ya mafuta husani kwa nchi zisizozalisha mafuta, ukame kwa baadhi ya maeneo na migogoro ya kisiasa kulisababisha kupungua kwa ukuaji wa uchumi Barani Afrika. Aidha, Pato la nchi za Afrika Kusini mwa Jangwa la Sahara lilikua kwa wastani wa asilimia 6.1 mwaka 2008 ikilinganishwa na asilimia 6.8 mwaka 2007.

**Ushirikiano wa Kiuchumi wa Kikanda na Kimataifa**

27. **Mheshimiwa Spika**, ushirikiano wa Tanzania kimataifa na kikanda uliendelea kuimarika na hivyo kuendelea kulijengea taifa mazingira mazuri ya shughuli za kiuchumi na kijamii. Kanda hizo ni pamoja na za Jumuiya ya Afrika Mashariki, Jumuiya ya Maendeleo ya Nchi za Kusini mwa Afrika (SADC), Mpango Mpya wa Ushirikiano wa Kuleta Maendeleo Afrika (NEPAD) pamoja na Shirika la Kimataifa la Biashara (WTO).

## Jumuiya ya Afrika Mashariki

28. **Mheshimiwa Spika,** katika mwaka 2008, Jumuiya ya Afrika Mashariki iliendelea na majadiliano ya kuunda Soko la Pamoja la Jumuiya ambalo linatarajiwa kuanza kutekelezwa mwaka 2010. Vile vile, katika jitihada za kuimarisha ushirikiano, mkataba wa ujenzi wa barabara ya Arusha - Namanga hadi Athi River (Kenya) ulisainiwa mwaka 2008. Aidha, miradi kwa ajili ya kuimarisha upatikanaji wa umeme kati ya Kenya na Tanzania ilianza katika miji ya Longido na Namanga.

## Jumuiya ya Maendeleo ya Nchi za Kusini mwa Afrika

29. **Mheshimiwa Spika,** katika mwaka 2008, Mpango wa kuwa na Eneo Huru la Biashara (SADC – FTA) ulizinduliwa katika mji wa Sandston, Afrika ya Kusini na ulianza rasmi Januari 2008. Mpango huu unatoa fursa ya kufanya biashara bila ushuru katika Kanda kwa asilimia 85. Aidha, Wakuu wa Nchi na Serikali za Jumuiya ya Maendeleo ya Nchi za Kusini mwa Afrika, Jumuiya ya Soko la Pamoja la Nchi za Mashariki, na Kusini mwa Afrika (COMESA); na Jumuiya ya Afrika Mashariki walifanya Mkutano wa pamoja kwa lengo la kuendeleza muungano wa jumuiya hizo. Wakuu wa nchi walikubaliana kuanzisha Eneo Huru la Biashara ambalo litajumuisha Jumuiya zote tatu na hatimaye kuwa na umoja wa forodha.

**Mpango Mpya wa Ushirikiano wa Kuleta Maendeleo Afrika (NEPAD)**

30. **Mheshimiwa Spika,** katika mkutano wa Wakuu wa Nchi za Jumuiya ya Afrika uliofanyika Juni 2008, Wakuu wa Nchi na Kamati ya Utekelezaji wa NEPAD walikubaliana kuhusu mapitio ya utekelezaji wa NEPAD kwa lengo la kuharakisha utengemazi wa NEPAD kwenye mfumo wa Jumuiya ya Afrika. Aidha, iliamuliwa kuwa mchakato na masuala yote ya utengemazi wa NEPAD kwenye mfumo wa Jumuiya ya Afrika uwe umekamilika kabla ya kikao cha kawaida cha 20 cha Wakuu wa Nchi na Serikali wa Kamati ya Utekelezaji wa NEPAD.

**Shirika la Kimataifa la Biashara**

31. **Mheshimiwa Spika,** Tanzania iliendelea kushiriki na kuunga mkono majadiliano ya biashara baina ya nchi wanachama wa Shirika la Kimataifa la Biashara. Hata hivyo, majadiliano yalivunjika Julai 2008 baada ya kushindwa kufikiwa muafaka kati ya Nchi Zilizoendelea na Nchi Zinazoendelea juu ya suala la utoaji wa ruzuku ya mazao ya kilimo kwa Nchi Zilizoendelea wakati Nchi Zinazoendelea zinashinikiza kupunguza ruzuku katika mazao.

## MAENDELEO YA SHUGHULI MBALIMBALI ZA KIUCHUMI NA KIJAMII

32. **Mheshimiwa Spika,** Mawaziri wa maeneo husika wataeleza kwa kina maendeleo katika maeneo yao; hivyo katika hotuba hii, nitaelezea kwa kifupi kuhusu maendeleo ya maeneo hayo.

### Kilimo, Mifugo, Misitu na Uwindaji

33. **Mheshimiwa Spika,** kiwango cha ukuaji katika shughuli za kiuchumi za kilimo, mifugo, misitu na uwindaji kiliongezeka kwa asilimia 4.6 mwaka 2008 ikilinganishwa na kiwango cha asilimia 4.0 mwaka 2007. Ukuaji huu ulitokana na kuongezeka kwa uzalishaji wa mazao kufuatia kuwepo kwa hali nzuri ya hewa katika msimu wa kilimo wa mwaka 2007/08; kuimarika kwa miundombinu ya umwagiliaji na barabara vijijini; jitihada za Serikali za kuwasambazia wakulima pembejeo za kilimo kama mbolea ya ruzuku na zana za kilimo; na kuhimiza ufugaji wa kibiashara.

34. **Mheshimiwa Spika,** kiwango cha ukuaji katika shughuli ndogo za uzalishaji mazao kiliongezeka kutoka asilimia 4.5 mwaka 2007 hadi asilimia 5.1 mwaka 2008. Kwa kuzingatia mabadiliko ya mgawanyo wa mazao na mahitaji yake, utaratibu uliokuwa ukitumika awali wa kugawa

mazao katika makundi mawili: ya chakula na biashara kwa sasa hautumiki tena, kwani sehemu kubwa ya mazao ambayo yalikuwa yanajulikana kama ya chakula yaliuzwa hususan katika nchi za jirani. Kiwango cha ukuaji katika shughuli ndogo za mifugo kiliongezeka kutoka asilimia 2.4 mwaka 2007 hadi asilimia 2.6 mwaka 2008. Sababu zilizochangia katika ukuaji huo ni pamoja na: upatikanaji wa malisho ya kutosha; na kuongezeka kwa huduma za ugani katika shughuli za uendelezaji kilimo na mifugo. Shughuli ndogo za kiuchumi katika misitu na uwindaji zilikua kwa kiwango cha asilimia 3.4 mwaka 2008, ikilinganishwa na asilimia 2.9 mwaka 2007. Hii ilitokana na kuongezeka kwa ada za uwindaji wa kitalii pamoja na ada za vibali vya kukamata wanyamapori hai.

35. **Mheshimiwa Spika,** kama nitakavyoeleza baadaye leo jioni katika hotuba ya bajeti, kaulimbiu ya serikali mwaka 2009/10 ni **"Kilimo Kwanza"** na bajeti itajielekeza zaidi katika kutekeleza hilo. Serikali inaendelea kufanya jitihada za kuboresha miundombinu ya umwagiliaji na barabara za vijijini, pamoja na utekelezaji wa Programu ya Kuendeleza Sekta ya Kilimo ili kuongeza kasi ya ukuaji wa sekta hiyo, na vile vile kupunguza athari za kuanguka kwa uchumi wa dunia katika uchumi wa Tanzania. Maeneo mengine yatakayopewa kipaumbele ni pamoja na kuongeza ubora wa bidhaa za kilimo na upatikanaji wa masoko; kuongeza

upatikanaji wa mikopo ya kilimo na yenye gharama nafuu; kuhakikisha upatikanaji kwa wakati wa pembejeo za kilimo kama vile mbolea, mbegu bora na zana za kilimo; kuendelea kuboresha upatikanaji wa chakula cha kutosha, kupanua kilimo cha umwagiliaji na kuongeza hifadhi ya Taifa ya chakula; kuimarisha ufanisi na upatikanaji wa huduma za ugani kwa wakulima na wafugaji; kuendelea kujenga na kukarabati mabwawa, majosho na machinjio ya mifugo; kuendeleza viwanda vya usindikaji mazao ya kilimo; kuongeza na kupanua wigo wa uzalishaji wa mazao ya kuuza nje; kupunguza uvunaji wa misitu usio endelevu na kushirikiana na wadau mbalimbali katika kuweka usimamizi endelevu wa misitu na vivutio vya utalii.

**Uvuvi**

36. **Mheshimiwa Spika,** shughuli za kiuchumi katika uvuvi zilikua kwa kiwango cha asilimia 5.0 mwaka 2008 ikilinganishwa na asilimia 4.5 mwaka 2007. Ongezeko hilo lilitokana na udhibiti wa uvuvi haramu; na uboreshwaji wa mazingira ya mazalia ya samaki. Mchango wa shughuli za uvuvi katika Pato la Taifa ulipungua kidogo na kufikia asilimia 1.2 mwaka 2008 kutoka asilimia 1.3 mwaka 2007.

37. **Mheshimiwa Spika,** katika kipindi cha mwaka 2009/10, maeneo ya kipaumbele yatakuwa ni: kupitia upya Sera ya Uvuvi ya mwaka 1997 ili kuweza kukabiliana na changamoto zilizopo; kuendelea kukabiliana na uvuvi haramu; na kuhakikisha upatikanaji wa vifaa bora vya kuhifadhi samaki.

**Viwanda na Ujenzi**

38. **Mheshimiwa Spika,** kiwango cha ukuaji wa uzalishaji bidhaa viwandani kilikuwa asilimia 9.9 mwaka 2008 ikilinganishwa na asilimia 8.7 mwaka 2007. Ukuaji huu ulitokana hasa na kuongezeka kwa uzalishaji wa bidhaa viwandani hususan bidhaa za chakula na maziwa, kemikali na uchapishaji; na kuongezeka kwa uzalishaji wa bidhaa zilizouzwa nje. Mchango wa shughuli za uzalishaji bidhaa viwandani katika Pato la Taifa ulikuwa asilimia 7.8 mwaka 2008, sawa na ilivyokuwa miaka miwili iliyotangulia.

39. **Mheshimiwa Spika,** katika kipindi cha muda wa kati, maeneo yatakayopewa kipaumbele katika uzalishaji viwandani ni pamoja na kuendeleza viwanda vya msingi, kuongeza thamani ya bidhaa na kupunguza uuzaji wa mazao ghafi nje.

40. **Mheshimiwa Spika,** shughuli za kiuchumi katika ujenzi zilikua kwa asilimia 10.5 mwaka 2008 ikilinganishwa na asilimia 9.7 mwaka 2007. Ukuaji huo ulichangiwa hasa na kuongezeka kwa shughuli za ujenzi wa barabara na madaraja; majengo ya kuishi na yasiyo ya kuishi; na upanuzi wa miundombinu ya maji. Mchango wa shughuli za ujenzi katika Pato la Taifa ulikuwa asilimia 7.7 mwaka 2008 ukilinganisha na asilimia 7.8 mwaka 2007. Malengo ya mwaka 2009/10 ni pamoja na kuendeleza ujenzi wa barabara kama ilivyobainishwa katika ilani ya uchaguzi ya CCM ya mwaka 2005.

41. **Mheshimiwa Spika,** kiwango cha ukuaji wa shughuli za kiuchumi katika umeme na gesi kilikuwa asilimia 5.4 mwaka 2008 ikilinganishwa na asilimia 10.9 mwaka 2007. Upungufu huo ulitokana na kupungua kwa ufuaji wa umeme wa gesi na makaa ya mawe na kumalizika kwa muda wa mikataba ya Dowans, APR na Aggreko. Shughuli za kiuchumi katika umeme na gesi zilichangia asilimia 1.7 katika Pato la Taifa mwaka 2008 ikilinganishwa na asilimia 1.6 mwaka 2007.

42. **Mheshimiwa Spika,** katika kipindi cha muda wa kati, juhudi zitaelekezwa katika ufuaji umeme, usafirishaji na usambazaji na kuongeza upatikanaji wa nishati ya kisasa vijijini. Aidha, serikali itaendelea na

mchakato wa kuanzisha Hifadhi ya Taifa ya Mafuta na upanuzi wa miundombinu ya gesi ya Songo Songo na Mnazi Bay.

43. **Mheshimiwa Spika,** ukuaji katika shughuli za kiuchumi za madini na uchimbaji mawe ulishuka kutoka asilimia 10.7 mwaka 2007 hadi asilimia 2.5 mwaka 2008. Upungufu huo ulitokana na kushuka kwa uzalishaji katika migodi mikubwa kulikosababishwa na mambo kadhaa, ikiwa ni pamoja na kuharibika kwa sehemu ya miundombinu ya uchimbaji katika mgodi wa dhahabu wa Geita ambao ndiyo mkubwa kuliko yote nchini, kuliathiri uzalishaji wa dhahabu kwa kiasi kikubwa. Aidha, mabadiliko ya umiliki wa mgodi wa almasi wa Williamson, ambapo kasi ya uzalishaji katika kipindi cha mpito kwa wamiliki wapya ilipungua na vile vile walisitisha uuzaji wa almasi nje. Mchango wa shughuli za kiuchumi za madini na uchimbaji mawe katika Pato la Taifa ulipungua kutoka asilimia 3.5 mwaka 2007 hadi asilimia 3.4 mwaka 2008.

44. **Mheshimiwa Spika,** Serikali itaendelea kuifanyia marekebisho Sera ya Madini ili kuiwezesha sekta ya madini kutoa mchango mkubwa katika ukuaji wa Pato la Taifa. Maboresho katika sekta ya madini yatalenga katika kuongeza ushirikishwaji wa wananchi, kuboresha mfumo wa sheria na kodi na pia kuwajengea uwezo wachimbaji wadogo.

**Huduma za Kiuchumi**

45. **Mheshimiwa Spika,** shughuli za utoaji huduma zinajumuisha biashara na matengenezo; uchukuzi; mawasiliano; hoteli na migahawa; utawala; elimu; afya; huduma za fedha na bima; na upangishaji wa majengo. Kiwango cha ukuaji wa shughuli za kiuchumi katika utoaji huduma kilikua kwa asilimia 8.5 mwaka 2008 ikilinganishwa na asilimia 8.1 mwaka 2007. Mchango wa shughuli za utoaji huduma katika Pato la Taifa ulikuwa asilimia 43.7 mwaka 2008 ikilinganishwa na asilimia 43.3 mwaka 2007.

46. **Mheshimiwa Spika,** shughuli za mawasiliano katika mwaka 2008 zilikua kwa kiwango kikubwa zaidi kuliko shughuli nyingine zote za huduma za kiuchumi. Kiwango cha ukuaji kwa shughuli hizi kilikuwa asilimia 20.5 mwaka 2008 ikilinganishwa na asilimia 20.1 mwaka 2007. Ukuaji huu ulichangiwa na kuongezeka kwa wateja wa huduma za mawasiliano ya simu za mkononi. Mchango wa shughuli za mawasiliano katika Pato la Taifa uliongezeka hadi kufikia asilimia 2.5 mwaka 2008 ikilinganishwa na asilimia 2.3 mwaka 2007.

47. **Mheshimiwa Spika,** shughuli za huduma za uchukuzi zilikua kwa kiwango cha asilimia 6.9 mwaka 2008 ikilinganishwa na asilimia 6.5 mwaka 2007. Ukuaji huu ulitokana na kuongezeka kwa kiasi cha mizigo iliyosafirishwa kwa njia ya barabara na kuongezeka kwa abiria katika safari za anga za kimataifa. Mchango wa huduma za uchukuzi katika Pato la Taifa umeendelea kuwa asilimia 4.2 mwaka 2008 sawa na ilivyokuwa mwaka 2007.

48. **Mheshimiwa Spika,** katika mwaka 2009/10, kipaumbele katika shughuli za kiuchumi za mawasiliano na uchukuzi kitawekwa kwenye kuendeleza miundombinu ya usafirishaji pamoja na kuongeza kasi ya ushirikishwaji wa sekta binafsi na jamii kwa ujumla katika kuendeleza shughuli hizi. Aidha, Serikali itaendelea kutekeleza mradi wa mkongo wa Taifa.

49. **Mheshimiwa Spika,** shughuli za biashara na matengenezo zilikua kwa asilimia 10.0 mwaka 2008 ikilinganishwa na asilimia 9.8 mwaka 2007. Ukuaji huo ulitokana na kuimarika kwa biashara nchini. Shughuli ndogo za biashara na matengenezo zilichangia asilimia 11.6 ya Pato la Taifa mwaka 2008 ikilinganishwa na asilimia 11.5 mwaka 2007.

50. **Mheshimiwa Spika,** shughuli ndogo za mahoteli na migahawa (ikijumuisha utalii) zilikua kwa asilimia 4.5 mwaka 2008 ikilinganishwa na asilimia 4.4 mwaka 2007. Ukuaji huo ulitokana na mikakati ya kutangaza vivutio vya utalii ndani na nje ya nchi. Mchango wa shughuli za huduma za mahoteli na migahawa katika Pato la Taifa ulishuka kidogo kufikia asilimia 2.6 mwaka 2008 ikilinganishwa na asilimia 2.7 mwaka 2007. Katika kipindi cha muda wa kati, Serikali itaendelea kuboresha sekta ya utalii kwa Kuhimiza utalii wa ndani; kutangaza vivutio vya utalii wetu nje; na kutafuta masoko hususan nchi za Asia.

51. **Mheshimiwa Spika,** shughuli za huduma za kifedha zilikua kwa asilimia 11.9 mwaka 2008 ikilinganishwa na asilimia 10.2 mwaka 2007. Ukuaji huu ulitokana na kuongezeka kwa mahitaji ya mikopo kwa sekta binafsi; mahitaji ya kifedha kwa ajili ya uwekezaji; huduma za bima; na huduma za kibiashara. Mchango wa shughuli za huduma za kifedha katika Pato la Taifa ulikuwa asilimia 1.6 mwaka 2008 sawa na ilivyokuwa mwaka 2007.

52. **Mheshimiwa Spika,** ukuaji wa huduma za upangishaji majengo na huduma za biashara ulikuwa asilimia 7.1 mwaka 2008 ikilinganishwa na asilimia 7.0 mwaka 2007. Mchango wa shughuli za upangishaji majengo na huduma za biashara katika Pato la Taifa ulikuwa asilimia 9.6 mwaka 2008 ikilinganishwa na asilimia 9.5 mwaka 2007.

53. **Mheshimiwa Spika,** katika mwaka 2008, shughuli za utawala zilikua kwa asilimia 7.0 ikilinganishwa na asilimia 6.7 mwaka 2007. Ukuaji huu ulitokana na kuendelea na utekelezaji wa awamu ya pili ya Programu ya Maboresho ya Sekta ya Umma. Mchango wa shughuli za utawala katika Pato la Taifa ulikuwa asilimia 8.2 mwaka 2008 ikilinganishwa na asilimia 7.9 mwaka 2007.

54. **Mheshimiwa Spika,** kiwango cha ukuaji katika shughuli za huduma ya elimu kilikuwa asilimia 6.9 mwaka 2008 ikilinganishwa na asilimia 5.5 mwaka 2007. Ukuaji katika shughuli hizi ulitokana na kuendelea na utekelezaji wa Awamu ya Pili ya Mpango wa Maendeleo ya Elimu ya Msingi (MMEM II); Mpango wa Maendeleo ya Elimu ya Sekondari (MMES); na kuongezeka kwa ajira mpya za walimu. Mchango wa shughuli za huduma za elimu katika Pato la Taifa ulikuwa asilimia 1.3 mwaka 2008 ikilinganishwa na asilimia 1.4 mwaka 2007.

55. **Mheshimiwa Spika,** katika kipindi cha muda wa kati, juhudi zitaelekezwa katika maeneo yafuatayo:

(i) Kuboresha usimamizi wa mfumo wa mawasiliano katika sekta ya elimu.

(ii) Kuboresha utoaji wa elimu maalum; na

(iii) Kupanua na kuboresha miundombinu kwa ajili ya taasisi za elimu ya juu ili kukidhi mahitaji yatakayotokana na utekelezaji wa MMEM na MMES.

56. **Mheshimiwa Spika,** kiwango cha ukuaji katika huduma za afya kilikuwa asilimia 9.0 mwaka 2008 ikilinganishwa na asilimia 8.8 mwaka 2007. Aidha, ukuaji huu ulichangiwa na utekelezaji wa programu za chanjo, malaria, kifua kikuu na VVU na UKIMWI. Mchango wa shughuli za huduma za afya katika Pato la Taifa ulikuwa asilimia 1.5 mwaka 2008 ikilinganishwa na asilimia 1.6 mwaka 2007.

57. **Mheshimiwa Spika,** katika mwaka wa 2009/10 Serikali itaweka mkazo katika maeneo yafuatayo:

(i) Kuendelea na utekelezaji wa Mpango wa Maendeleo wa Huduma ya Afya ya Msingi;

(ii) Kuimarisha upatikanaji wa huduma bora kwa akina mama wajawazito na watoto chini ya umri wa miaka mitano; na

(iii) Kuendelea na utekelezaji wa Mpango wa Taifa wa VVU na UKIMWI.

## MASUALA MTAMBUKA

### *Idadi ya Watu*

58. **Mheshimiwa Spika,** kulingana na makadirio ya kiwango cha ukuaji wa idadi ya watu cha asilimia 2.9 cha Sensa ya Watu na Makazi ya mwaka 2002, idadi ya watu Tanzania ilikadiriwa kuwa milioni 40.7 mwaka 2008. Kati yao, watu milioni 20.7 sawa na asilimia 50.9 walikuwa ni wanawake na watu milioni 20.0 sawa na asilimia 49.1 walikuwa ni wanaume. Tanzania Bara ilikadiriwa kuwa na jumla ya watu milioni 39.5 na Tanzania Zanzibar watu milioni 1.2.

59. **Mheshimiwa Spika,** mchanganuo wa idadi ya watu kulingana na umri ni kama ifuatavyo: watu wenye umri chini ya miaka 15 ni asilimia 44.4 ya watu wote; watu wenye umri kati ya miaka 15 hadi 24 ni asilimia

19.8; idadi ya watu wenye umri kati ya miaka 25 hadi 64 ni asilimia 32.4; na watu wenye umri zaidi ya miaka 65 walikuwa ni asilimia 3.4 ya watu wote.

***Nguvukazi na Ajira***

60. **Mheshimiwa Spika,** katika mwaka 2008, nguvukazi nchini iliendelea kuwa watu milioni 20.6 kulingana na matokeo ya Utafiti wa Watu wenye Uwezo wa Kufanya Kazi (Integrated Labour Force Survey - ILFS) wa mwaka 2005/06. Vile vile, matokeo hayo yanaonyesha kuwa watu milioni 18.3 walikuwa wana ajira. Kati yao, watu milioni 9.0 walikuwa wanaume na wanawake walikuwa milioni 9.3. Katika mwaka 2008, Serikali ilianzisha Wakala wa Huduma za Ajira ili kusaidia kutoa huduma bora zinazohusu ajira hapa nchini ikiwa ni pamoja na kuwaunganisha watu wanaotafuta kazi na waajiri ndani na nje ya nchi.

**Utawala Bora**

61. **Mheshimiwa Spika,** mwaka 2008, Serikali iliendelea kuboresha taratibu za uchaguzi na kuimarisha demokrasia nchini kwa kuanza kuhuisha Sheria ya Uchaguzi Sura 343 na Sheria ya Serikali za Mitaa Sura 292. Aidha, katika mwaka 2008, Tume ya Uchaguzi ilianza zoezi la kuhakiki daftari la wapiga kura nchini. Lengo ni kurekebisha taarifa za wapiga kura kwa waliohama kutoka sehemu moja kwenda nyingine, kuwasajili

waliofikisha umri wa kupiga kura, na kuwaondoa waliopoteza sifa za kupiga kura na waliofariki.

62. **Mheshimiwa Spika,** katika mwaka 2008, Serikali ilianza kufanya utafiti wa kutathmini hali ya rushwa na utawala bora nchini (National Governance and Corruption Survey) na matokeo ya utafiti huu yatatolewa mwishoni mwa mwezi Juni 2009.

63. **Mheshimiwa Spika,** katika kuboresha shughuli za Mahakama, mwaka 2008, Majaji wapya 15 waliteuliwa; Mahakimu Wakazi na wa Wilaya 95; na Mahakimu wa Mahakama za Mwanzo 128 waliajiriwa. Kufuatia kuongezeka kwa watumishi hao, Mahakama ya Rufaa iliweza kusikiliza mashauri 1,189 kati ya 3,043 yaliyokuwepo. Mahakama Kuu ilisikiliza mashauri 4,683 kati ya mashauri 14,152 yaliyokuwepo. Kwa upande wa Mahakama za Mikoa na Wilaya, jumla ya mashauri 30,615 yalipangwa kusikilizwa na kati ya hayo mashauri 17,595 yalisikilizwa. Mahakama ya Biashara ilisikiliza mashauri ya kibiashara 117 yaliyofunguliwa na mashauri 90 yalitolewa maamuzi. Mahakama ya Kazi ilikamilisha mashauri 364 yanayohusu migogoro ya kazi kati ya mashauri 577.

64. **Mheshimiwa Spika,** katika mwaka 2007/08, Wakala wa Usajili, Ufilisi, na Udhamini (RITA) ulisajili jumla ya vizazi 2,268,272; vifo 117,295; na ndoa 12,295; ikilinganishwa na vizazi 829,384; vifo 118,538 na ndoa 46,320 mwaka 2006/07 kwa mtiririko huo. Aidha, jumla ya watoto 27 wa kuasiliwa waliandikishwa na kupata vyeti.

**Mazingira**

65. **Mheshimiwa Spika,** katika kupambana na uharibifu wa mazingira, Serikali iliendelea kutekeleza sera, mikakati, sheria na kanuni zinazolenga kuwa na utumiaji endelevu wa mazingira kwa ajili ya maendeleo ya kiuchumi na kijamii. Utekelezaji wa shughuli za mazingira katika mwaka 2008, ulikuwa kama ifuatavyo: Wilaya 37 zilivuka lengo la kupanda miti milioni 1.5; Taarifa ya hali ya mazingira nchini kwa kipindi cha mwaka 2007/08 ilikamilika; Mikataba ya kimataifa kuhusu mabadiliko ya tabianchi; na mradi wa usimamizi wa bonde la Ziwa Tanganyika ulianza kutekelezwa.

**Vita Dhidi ya UKIMWI**

66. **Mheshimiwa Spika,** janga la UKIMWI limeendelea kuwa ni tishio kwa maendeleo ya Taifa. Athari zake zimeendelea kusambaa kwa familia na jamii. Katika mwaka 2007/08, watu wanaoishi na VVU wenye umri kati ya miaka 15 - 49 walikadiriwa kuwa asilimia 5.7. Kasi ya maambukizi ya

UKIMWI inakadiriwa kuwa asilimia 5.8, ambapo maambukizi kwa wanawake ni asilimia 6.6 na wanaume asilimia 4.6. Mwaka 2008, idadi ya watu wanaoishi na VVU na wanaopata tiba ya madawa ya kupunguza makali ya UKIMWI iliongezeka hadi watu 193,978 kutoka watu 69,250 mwaka 2007.

67. **Mheshimiwa Spika,** mwaka 2008, Serikali iliendelea kutekeleza Mpango Mkakati wa Pili wa Sekta mbalimbali juu ya VVU na UKIMWI kwa kipindi cha mwaka 2008-2012. Mpango huo unalenga katika kuelekeza njia mbalimbali za kudhibiti maambukizi ya UKIMWI. Aidha, mwaka 2008, Mkakati wa kuzuia maambukizi kutoka kwa mama kwenda kwa mtoto ulipanuliwa hadi katika ngazi za vituo vya msingi vya afya nchini. Mkakati huo unalenga kuwa na watoto wanaozaliwa ambao hawajaambukizwa.

**Jinsia**

68. **Mheshimiwa Spika,** katika mwaka 2008, Serikali iliendelea kuweka msisitizo katika kuingiza masuala ya jinsia katika sera za kisekta na zile za jumla. Katika kufanikisha hilo, mafunzo ya uingizaji masuala ya jinsia katika maeneo hayo yalitolewa kwa watendaji mbalimbali wakiwemo Makatibu Wakuu wa Wizara, waratibu wa jinsia katika wizara na kamati za jinsia za kisekta.

69. **Mheshimiwa Spika,** Serikali iliendelea kutekeleza mikataba ya kikanda na kimataifa kuhusu maendeleo ya jinsia kwa kuongeza ushiriki wa wanawake katika ngazi mbalimbali za uongozi wa kisiasa, kiutendaji na nafasi za maamuzi kwa lengo la kufikia uwiano wa kijinsia. Aidha, Serikali imetafsiri Azimio kuhusu usawa wa jinsia Afrika (Solemn Declaration on Gender Equality in Africa) na Mkataba wa Kuondoa Aina Zote za Unyanyasaji wa Wanawake katika lugha rahisi (popular version) kwa lengo la kuwafikishia ujumbe walengwa.

**Msukosuko wa Uchumi Duniani na Athari zake kwa Uchumi wa Tanzania**

70. **Mheshimiwa Spika,** chimbuko la msukosuko wa uchumi duniani lilitokana na watu wengi nchini Marekani kushindwa kurejesha mikopo ya nyumba kufuatia kupanda kwa riba na kusababisha sekta ya fedha kuvurugika. Aidha, hali hii ilisababisha kuporomoka kwa masoko ya fedha na mitaji nchini Marekani na kusambaa katika masoko ya fedha na mitaji ya nchi zilizoendelea na zinazoinukia kiuchumi. Kutokana na msukosuko huu, Shirika la Fedha la Kimataifa (IMF) linakisia ukuaji hasi wa asilimia 1.3 kwa uchumi wa dunia kwa mwaka 2009. Hali hii imesababishwa na ukuaji hasi wa wastani wa asilimia 3.8 kwa nchi zilizoendelea. Aidha, ukuaji wa

pato kwa nchi zinazoinukia na zinazoendelea utashuka kutoka wastani wa asilimia 6.1 mwaka 2008 hadi wastani wa asilimia 1.6 mwaka 2009. Pato la nchi za Afrika litashuka hadi asilimia 2.0 mwaka 2009 kutoka asilimia 5.9 mwaka 2008.

71. **Mheshimiwa Spika,** Serikali imekwishachukua hatua za awali za kupunguza au kukabiliana na athari za msukosuko huu wa uchumi. Kwa kuzingatia chanzo cha msukosuko huu, Benki Kuu imekuwa na utaratibu wa uangalizi na usimamizi wa mabenki kila siku ili kuweza kubaini matatizo yatakayojitokeza na kuchukua hatua za haraka. Aidha, katika kupunguza makali na kuhimili shinikizo la msukosuko hususan kuwalinda wananchi walio kwenye hatari kubwa zaidi, Serikali inalenga katika kutekeleza yafuatayo: kulinda ajira hasa katika baadhi ya shughuli zitakazokumbwa na matatizo ya ukwasi kutokana na kupungua kwa utashi wa bidhaa na huduma wanazozalisha; kuinusuru nchi kutokana na athari za upungufu wa chakula duniani zilizochochewa na msukosuko pamoja na hali mbaya ya hewa; kulinda programu muhimu za kijamii; na kulinda uwekezaji muhimu kwa maendeleo ya nchi.

## MIPANGO MAALUM YA MAENDELEO YA KIUCHUMI NA KIJAMII

72. **Mheshimiwa Spika,** katika kufikia malengo ya maendeleo ya kiuchumi na kijamii, Serikali imekuwa ikitekeleza mipango na programu mbalimbali za muda mrefu, kati na muda mfupi kama ifuatavyo:

**Dira ya Taifa ya Maendeleo 2025**

73. **Mheshimiwa Spika,** Dira ya Taifa ya Maendeleo 2025 ni mpango wa muda mrefu ambao unalenga kuwa ifikapo mwaka 2025, Tanzania iwe ni miongoni mwa nchi zenye viwango vya kati vya mapato (middle income country) na hali bora ya maisha. Mpango huu unalenga kwamba Tanzania ya mwaka 2025 iwe na sifa zifuatazo: maisha bora na mazuri; amani, utulivu na umoja; utawala na uongozi bora; jamii iliyoelimika na inayopenda kujifunza zaidi; na uchumi wenye uwezo wa ushindani na kujiletea ukuaji endelevu kwa maslahi ya watu wote. Tangu Dira hii kuanza kutekelezwa mwaka 2000, Serikali imekuwa ikiandaa mikakati ya muda wa kati ya utekelezaji wa Dira (Medium Term Plan) na kila sekta inaagizwa kuandaa mpango mkakati (strategic plan) wa kufikia malengo ya Dira. Pia kulikuwepo na mkakati wa kitaifa wa kupunguza umaskini (PRS I) ambao utekelezaji wake ulifanyika kwa ufanisi katika kipindi cha mwaka 2000/01 – 2003/04. Utekelezaji wa Dira unaendelea kupitia mipango, mikakati na programu mbalimbali za muda wa kati na muda mfupi ikiwemo: Mkakati wa Kukuza Uchumi na Kupunguza Umaskini Tanzania (MKUKUTA); Mfuko

wa Maendeleo ya Jamii (TASAF); na Mpango Maalum wa Kuharakisha Maendeleo ya Tanzania 2020 (Mini-Tiger Plan 2020). Baada ya miaka kumi ya utekelezaji wa Dira, Serikali inafanya tathmini ili kujua mafanikio na changamoto zilizojitokeza na mikakati ya kuzikabili. Zoezi hilo linaendelea na taarifa rasmi itawasilishwa serikalini na mshauri mwelekezi mwishoni mwa Juni, 2009.

**Mkakati wa Kukuza Uchumi na Kupunguza Umaskini Tanzania (MKUKUTA)**

74. **Mheshimiwa Spika,** kwa ujumla, utekelezaji wa MKUKUTA ambao unalenga kufikia malengo ya Dira 2025 umekuwa na mafanikio katika maeneo yake yote matatu. Katika kipindi cha mwaka 2007/08, viashiria vinaonesha kuwa kumekuwa na ongezeko katika ukuaji wa Pato la Taifa; ukusanyaji wa mapato ya ndani, na kuimarika kwa miundombinu hasa ya barabara. Ukuaji huu umejidhihirisha katika kupungua kwa umaskini.

75. **Mheshimiwa Spika,** utafiti wa Mapato na Matumizi ya Kaya kwa Tanzania Bara uliofanyika mwaka 2007 unaonesha kuwa idadi ya watanzania wasiojitosheleza kwa mahitaji ya msingi imeshuka kutoka asilimia 35.6 mwaka 2000/01 hadi asilimia 33.4 mwaka 2007 na wasiojitosheleza kwa chakula imepungua kutoka asilimia 18.7 mwaka

2000/01 hadi asilimia 16.5 mwaka 2007. Hata hivyo, Serikali inaona kuwa kasi ya kupungua kwa umaskini hairidhishi, hivyo, hatua zitachukuliwa za kuongeza kasi ya kupunguza umaskini.

76. **Mheshimiwa Spika,** katika kipindi cha mwaka 2007/08, mafanikio pia yalipatikana katika sekta za huduma ya jamii. Miongoni mwa mafanikio hayo ni: kuongezeka kwa uandikishaji wanafunzi katika shule za awali kutoka 795,011 mwaka 2007 hadi 873,981 mwaka 2008; msingi kutoka 8,316,925 mwaka 2007 hadi 8,410,094 mwaka 2008; sekondari kutoka 829,094 mwaka 2007 hadi 1,035,373 mwaka 2008 na vyuo vya elimu ya juu kutoka 60,716 mwaka 2007 hadi 100,394; kuongezeka kwa idadi ya wanafunzi wanaojiunga na shule za sekondari; kuongezeka kwa idadi ya wanafunzi wa elimu ya juu waliopatiwa mikopo; kuboreshwa kwa huduma za afya; na upatikanaji wa maji safi na salama mijini na vijijini .

77. **Mheshimiwa Spika,** pamoja na mafanikio hayo, kumekuwepo na changamoto kadhaa ambazo ni pamoja na: kutokuwepo kwa uwiano mzuri kati ya wanafunzi na walimu katika shule; mazingira yasiyoridhisha ya kujifunzia na kufundishia; kutokuwepo kwa uwiano sawa wa kijinsia hasa katika shule za sekondari na elimu ya juu; na kiwango cha juu cha vifo vya

mama wajawazito na watoto. Serikali inachukua hatua za kurekebisha hali hii kulingana na uwezo wake.

78. **Mheshimiwa Spika,** katika suala la utawala bora na uwajibikaji, vyombo vinavyohusika na haki za binadamu vimefanya kazi nzuri hadi sasa na vitaendelea kuongezewa uwezo wa kiutendaji. Aidha, Serikali iliendelea na jitihada za kuhakikisha kuwa haki za binadamu zinalindwa.

**Mfuko wa Maendeleo ya Jamii (TASAF)**

79. **Mheshimiwa Spika,** katika utekelezaji wa shughuli za Mfuko wa Maendeleo ya Jamii (TASAF), jumla ya miradi 2,750 iliibuliwa Tanzania Bara na Tanzania Zanzibar katika kipindi cha Januari hadi Desemba 2008. Kati ya miradi hiyo, miradi 2,210 ilipatiwa fedha kwa ajili ya utekelezaji. Hadi mwishoni mwa Desemba 2008, jumla ya miradi 5,657 yenye thamani ya shilingi bilioni 126.2 iliibuliwa tangu TASAF awamu ya pili ianze. Kati ya miradi hiyo, miradi 3,700 ilikuwa kwa ajili ya jamii zenye ukosefu wa huduma za kijamii, miradi 1,628 kwa ajili ya makundi maalum na miradi 349 kwa ajili ya kaya zenye upungufu wa chakula lakini zina watu wenye uwezo wa kufanya kazi. Awamu ya pili ya TASAF inatekelezwa katika Halmashauri 133 za Tanzania Bara na Zanzibar.

**Mpango Maalum wa Kuharakisha Maendeleo ya Tanzania**

80. **Mheshimiwa Spika**, Mwaka 2004, Serikali ilitayarisha 'Mpango Maalumu wa Kuharakisha Maendeleo ya Tanzania (Tanzania Mini Tiger Plan 2020) kwa kuzingatia uzoefu na mafanikio ya nchi za Kusini Mashariki mwa Asia. Uzoefu wa nchi hizi unafaa kwa maendeleo ya Taifa letu kwa kuwa miaka takriban arobaini iliyopita baadhi ya nchi hizo zilikuwa sawa na Tanzania kimaendeleo na nyingine hata kuwa nyuma, lakini pamoja na hatua nyingine, kwa kuanzisha mipango maalum iliyobuniwa kuvutia uwekezaji, nchi hizi zimeweza kupiga hatua kubwa sana ya maendeleo.

81. **Mheshimiwa Spika**, lengo la Mpango huu ni kuanzisha maeneo maalum ya uwekezaji kwa ajili ya shughuli za viwanda, kilimo, utalii, upandaji miti, na TEKNOHAMA. Mojawapo ya maeneo hayo ni ujenzi wa eneo maalum la uwekezaji la Benjamini William Mkapa Special Economic Zone (BWM-SEZ) lililoko Mabibo Dar es Salaam ambao umefikia hatua za mwisho na unatarajiwa kukamilika ifikapo mwishoni mwa Juni 2009. Taratibu za kupata wawekezaji katika eneo husika zimeshaanza na tayari maombi ishirini yamekwishapokelewa kutoka kwa wawekezaji mbalimbali na yanashughulikiwa kulingana na vigezo vilivyoainishwa na mamlaka husika. Eneo hili litakapokamilika litakuwa na uwezo wa kutoa ajira mpya zisizopungua 20,000. Aidha, Kampuni za Oji Paper na Marubeni za Japan kwa kushirikiana na chuo cha Utafiti cha Naliendele tayari zimeshaanza

miradi ya kupanda miti kwenye mashamba ya majaribio katika mikoa ya Mtwara na Lindi. Lengo ni kuotesha misitu ya mbao kwa ajili ya kutengeneza karatasi ambazo zina soko kubwa duniani.

**Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi**

82. **Mheshimiwa Spika,** katika kutekeleza Sera ya Taifa ya Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi, mafanikio yamepatikana katika utoaji wa mikopo na uanzishwaji wa SACCOS na vikundi vidogo vidogo vya kiuchumi vya vijana na wanawake. Mikopo hiyo ilitolewa kupitia mifuko na programu mbalimbali ikijumuisha Programu ya Taifa ya Kuongeza Kipato; Mpango wa Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi na Kuongeza Ajira; Mfuko wa Uwezeshaji Mwananchi; na Mradi wa Kuhudumia Biashara Ndogo Ndogo (SELF).

83. **Mheshimiwa Spika,** hadi Machi 2009, awamu ya kwanza ya Mpango wa Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi na Kuongeza Ajira kupitia Mfuko wa Dhamana kwa benki za NMB na CRDB ulitoa mikopo yenye thamani ya shilingi bilioni 42.48, ikiwa ni asilimia 37.0 zaidi ya lengo la shilingi bilioni 31.0. Jumla ya wajasiriamali 65,508 walinufaika na mikopo hiyo kupitia SACCOS 192 na vikundi 86.

84. **Mheshimiwa Spika,** awamu ya pili ya Mpango wa Uwezeshaji wa Wananchi Kiuchumi na Kuongeza Ajira ilizinduliwa mwezi Januari 2008. Katika awamu hii, jumla ya shilingi bilioni 9.9 zilitolewa kwa benki na asasi 12 za fedha ambazo zilikopesha fedha hizo kwa walengwa kwa kuzingatia masharti nafuu ya ukopeshaji yaliyoidhinishwa na Serikali. Pia kiasi cha shilingi milioni 600 zilitolewa kwa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kwa ajili hiyo. Katika awamu hii, mikopo yenye thamani ya shilingi bilioni 5.7 ilitolewa na benki na asasi za fedha zilizoidhinishwa kwa wajasiriamali 22,150 katika wilaya 21 ambazo hazikupata fedha katika awamu ya kwanza na wilaya 46 zilizopata chini ya kiwango.

85. **Mheshimiwa Spika,** Mfuko wa Uwezeshaji Mwananchi (Mwananchi Empowerment Fund) ulianzishwa kwa mujibu wa Sheria ya Uwezeshaji Namba 16 ya mwaka 2004. Mfuko huo ulizinduliwa Januari, 2008 ukiwa na kianzio cha Shilingi milioni 400. Madhumuni ya Mfuko huo ni kudhamini mikopo ya wajasiriamali (Wadogo, Kati na Wakubwa) ambao wanashindwa kupata mikopo kwenye benki za biashara kwa sababu ya kukosa dhamana.

86. **Mheshimiwa Spika,** hadi mwishoni mwa Machi, 2009 Mfuko ulitoa mikopo yenye thamani ya Shilingi milioni 1,280 kwa SACCOS 18 za mikoa ya Mtwara, Lindi, Manyara na Rukwa ambapo wajasiriamali 720

walinufaika. Mikopo hiyo ilielekezwa kwenye shughuli za uzalishaji mali hususan kilimo. Aidha, uhamasishaji wa wajasiriamali kujiunga katika SACCOS ulifanyika na kufanikiwa kuongeza idadi ya SACCOS kutoka 1,875 mwaka 2005 hadi SACCOS 4,780 mwaka 2008.

87. **Mheshimiwa Spika,** Serikali iliendelea kutekeleza Mradi wa Kuhudumia Biashara Ndogo Ndogo (SELF) ambao ulianzishwa kwa lengo la kuwawezesha Watanzania kupata mitaji, hususan walioko vijijini. Hadi Machi, 2009 mikopo yenye thamani ya shilingi billioni 19.2 ilikuwa imetolewa kupitia asasi ndogo za Fedha zipatazo 206 na walengwa 64,446 walikuwa wamenufaika na mikopo hiyo, kati ya hao asilimia 58 ni wanawake. Kwa wastani kiwango cha marejesho kutoka kwa asasi ndogo za fedha zilizokopeshwa kilikuwa asilimia 95.

88. **Mheshimiwa Spika,** kupitia mradi huo wa SELF, mafunzo mbalimbali yalitolewa kwa watendaji wapatao 1,889 kutoka katika asasi ndogo za fedha zikiwemo SACCOS 373 na mashirika yasiyo ya serikali (NGOs) 33. Katika idadi hii Asasi 85 ziko Unguja na Pemba.

89. **Mheshimiwa Spika,** kwa ujumla maeneo yatakayopewa kipaumbele katika kipindi cha 2009/10 ni pamoja na: kubuni mikakati

mbalimbali ya utekelezaji wa Sera; kutafuta vyanzo vya fedha na kuendelea kutoa mikopo yenye masharti nafuu kwa wajasiriamali; kuratibu na kutathmini shughuli za uwezeshaji wananchi kiuchumi; kuandaa mfumo wa ufuatiliaji wa utekelezaji wa Sera ya Taifa ya Uwezeshaji Kiuchumi; kutoa mafunzo kwa wajasiriamali; kubuni na kuratibu tafiti mbalimbali zinazolenga kuongeza tija; na kuboresha upatikanaji wa taarifa muhimu za masoko ya bidhaa.

**Uendelezaji wa Sekta Binafsi**

90. **Mheshimiwa Spika,** Serikali inatambua mchango wa sekta binafsi katika kukuza uchumi na kupunguza umaskini. Kwa kuzingatia hilo, hatua zinachukuliwa kuboresha mazingira ya kuziwezesha sekta binafsi kushiriki kikamilifu katika shughuli za kiuchumi. Miongoni mwa hatua hizo ni pamoja na utekelezaji wa programu mbalimbali kama vile MKURABITA na MKUMBITA. Hali kadhalika, kukamilika kwa Sera ya ubia kati ya sekta ya umma na binafsi (PPP Policy) kutasaidia katika kuharakisha maendeleo ya sekta binafsi na kuongeza mchango wake katika kukuza uchumi na kupunguza umaskini.

**MKURABITA**

91. **Mheshimiwa Spika,** Mpango wa Kurasimisha Rasimali na Biashara za wanyonge Tanzania (MKURABITA) ni mpango ulioanzishwa na Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, mwezi Novemba, 2004 ukilenga kuwapa nguvu kiuchumi, wananchi hasa wale wa kipato cha chini vijijini na mijini, kwa kuwaongezea uwezo wa kumiliki rasilimali na kufanya biashara katika mfumo rasmi wa kisasa, unaoendeshwa kwa mujibu wa sheria na kanuni rasmi za kiutawala. Utekelezaji wa MKURABITA umepangwa katika awamu nne na utekelezaji wa awamu ya pili yaani "Maandalizi ya Maboresho" ulikamilika mwaka 2008. Katika hatua hii, maeneo mbalimbali yalipendekezwa kufanyiwa maboresho katika azma ya kufikia malengo ya MKURABITA. Miongoni mwa mapendekezo hayo ni pamoja na kurasimisha umiliki wa ardhi, kuruhusu matumizi ya ardhi kwa matumizi ya maendeleo kiuchumi, na kurasimisha biashara kwa kuondoa vikwazo. Hatua ya tatu ya utekelezaji wa MKURABITA ambayo ni "Utekelezaji wa Maboresho" imeanza. Lengo kuu katika hatua hii ni kutekeleza hatua za maboresho zilizopendekezwa katika awamu ya pili.

**Uboreshaji wa Mazingira ya Biashara (MKUMBITA)**

92. **Mheshimiwa Spika,** kupitia Mpango wa Kuboresha Mazingira ya Biashara Tanzania (MKUMBITA), Serikali iliweka kipaumbele katika kurekebisha mfumo wa sera, sheria na taratibu katika maeneo ambayo

mazingira wezeshaji yanatoa nafasi ya pekee ya kuchangia maendeleo ya sekta binafsi. Ili kupunguza urasimu wa kufanya biashara nchini, Serikali itatekeleza Sheria ya Uandikishaji wa Shughuli za Biashara (BARA) ya mwaka 2007, ambayo inaanza kwa Halmashauri 24. Uzoefu utakaopatikana utasaidia katika kuelewa faida na changamoto zilizopo ili kupendekeza maboresho au mabadiliko katika Sheria hiyo au kanuni zake.

93. **Mheshimiwa Spika,** katika mwaka 2008, MKUMBITA uliendelea kuchangia kujenga uwezo wa Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi katika maeneo yanayohusu utekelezaji wa Sheria ya Ardhi Vijijini ya mwaka 1999 ili kuongeza kasi ya utekelezaji wa Sheria hiyo kwa lengo la kuharakisha upatikanaji wa hatimiliki za ardhi.

94. **Mheshimiwa Spika,** Miradi mingine katika eneo hili ambayo Serikali inaendelea kutekeleza ni pamoja na Mradi wa Vitambulisho vya Taifa. Mradi huu unaendelea na maelezo zaidi yatatolewa na Wizara husika wakati wa kuwasilisha hotuba ya Bajeti yake. Mradi mwingine ni wa upimaji wa ardhi ya vijiji 1,500 vilivyobaki.

**Baraza la Taifa la Biashara**

95. **Mheshimiwa Spika,** mwaka 2008, Baraza la Taifa la Biashara liliendelea na jitihada za kuboresha mazingira ya biashara na kuwawezesha

wananchi kiuchumi. Aidha, Baraza liliendesha majadiliano kati ya sekta ya umma na sekta binafsi jinsi ya kuboresha mazingira ya biashara. Baraza limefungua matawi mikoa yote na tayari Mabaraza ya Wilaya yameanzishwa kwa nia ya kuboresha mazingira ya Biashara katika ngazi husika.

96. **Mheshimiwa Spika,** katika kipindi cha mwaka 2008, Baraza la Taifa la Biashara lilifanya mikutano ifuatayo: mkutano wa tano wa Baraza la Taifa la Biashara kuhusu Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi; Mkutano wa tatu wa wawekezaji wa ndani (Local Investors' Round Table); na Mkutano wa saba wa wawekezaji wa Nje (International Investors' Round Table). Madhumuni ya mikutano hii ni kuhamasisha uwekezaji kutoka nje na ndani kwa kushirikisha sekta ya binafsi.

**Uwekezaji Mitaji ya Kigeni ya Moja kwa Moja**

97. **Mheshimiwa Spika,** thamani ya uwekezaji wa mitaji ya kigeni ya moja kwa moja iliongezeka kufikia Dola za Kimarekani milioni 695.5 mwaka 2008 ikilinganishwa na dola za Kimarekani milioni 653.4 mwaka 2007, sawa na ongezeko la asilimia 6.4. Aidha, nchi ya Uingereza iliendelea kuongoza katika nchi zenye miradi mingi ya uwekezaji mwaka 2008 ikiwa

na miradi 96; Kenya 72, China 50, India 39, Uholanzi 27, Marekani 24, na Afrika Kusini 20.

## MISINGI NA MALENGO YA UCHUMI NA MAENDELEO YA JAMII 2009/10-2011/12

98. **Mheshimiwa Spika,** katika mwaka 2009/10, kaulimbiu ya Serikali ni **"Kilimo Kwanza".** Serikali itaweka mkazo katika kupanua na kuboresha kilimo kwa mapana yake (mazao, mifugo, uvuvi, mazao ya misitu na nyuki, uwindaji, umwagiliaji, ushirika na masoko) ikiwa ni pamoja na kuhakikisha upatikanaji wa pembejeo (mbolea na madawa), uzalishaji wa mbegu bora, upatikanaji wa zana za kilimo, huduma za ugani na mikopo nafuu kwa ajili ya kilimo. Aidha, Serikali itatilia mkazo katika kuendeleza na kupanua miradi ya kilimo cha umwagiliaji. Vile vile, ufugaji utaendelezwa kwa kuendelea kujenga na kukarabati mabwawa, malisho, machinjio ya mifugo na kuendeleza viwanda vya kusindika nyama. Lengo la hatua hii ni kuhakikisha kuwa chakula cha kutosha kinapatikana nchini pamoja na kuongeza uzalishaji na ubora wa mazao ya kilimo na mifugo.

99. **Mheshimiwa Spika,** kufuatia kikao cha wadau wa kilimo kilichofanyika Dar es Salaam tarehe 2 –3 Juni, 2009 chini ya uenyekiti wa Mheshimiwa Rais Jakaya Mrisho Kikwete, Serikali imeamua kukipa

kipaumbele kilimo katika mapana yake kwa kuandaa nguzo kumi za mapinduzi ya kilimo (Ten Pillars of a Green Revolution in Tanzania) ambazo ni: Dira ya Kilimo Kwanza; Ugharamiaji wa Kilimo Kwanza; Mabadiliko ya Mkakati wa Kushughulikia Kilimo; Kuhuisha Muundo wa Taasisi za Kilimo; Ardhi; Vivutio vya Kilimo; Mageuzi ya Viwanda vya Kilimo; Sayansi, Teknolojia na Rasilimali Watu; Maendeleo ya Miundombinu; na Uhamasishaji wa Watanzania juu ya dhana ya Kilimo Kwanza. Kikao kilipitia nguzo hizo na kutoa mapendekezo yao. Kwa sasa, Baraza la Taifa la Biashara (TNBC) na Shirikisho la Maendeleo ya Sekta Binafsi (TPSF) wanaandaa mpango kazi wa kutekeleza mapendekezo hayo ili kuwasilishwa serikalini.

100. **Mheshimiwa Spika,** kwa kuzingatia kauli mbiu ya "Kilimo Kwanza", misingi ya malengo ya uchumi jumla na maendeleo ya jamii kwa kipindi cha muda wa kati (2009/10 – 2011/12), ni kama ifuatavyo:

(i) Kuendelea kutengamaza vigezo muhimu vya uchumi jumla, ikiwa ni pamoja na ukuaji wa Pato la Taifa; kudhibiti kasi ya upandaji bei; na kutengemaza viwango vya ubadilishanaji fedha;

(ii) Kuimarisha Hifadhi ya Chakula ili kuweza kununua mazao ya kutosha kulingana na mahitaji ya Taifa. Aidha, mikoa sita ya Mbeya,

Ruvuma, Rukwa, Iringa, Morogoro na Kigoma inayozalisha mazao ya chakula kwa wingi itapewa kipaumbele katika kupatiwa pembejeo za kilimo;

(iii) Kuendeleza sekta ya kilimo kwa kuhakikisha upatikanaji kwa wakati wa pembejeo za kilimo kama mbolea, mbegu bora na madawa ya kuua wadudu; kuongeza thamani na ubora wa bidhaa za kilimo na upatikanaji wa masoko; kuendeleza viwanda vya usindikaji mazao ya kilimo; kuimarisha na kuendeleza miundombinu ya umwagiliaji na kuhimiza matumizi endelevu ya skimu za umwagiliaji; kuongeza upatikanaji wa mikopo ya kilimo na yenye gharama nafuu; na kuimarisha ufanisi na upatikanaji wa huduma za ugani;

(iv) Kuendeleza mifugo ikiwa ni pamoja na kuendelea kujenga na kukarabati mabwawa, majosho na machinjio ya mifugo; kuboresha huduma za ugani na upatikanaji wa maeneo ya ufugaji; kuendelea kutoa elimu kuhusu ufugaji wa kisasa kwa wafugaji; kudhibiti magonjwa ya mifugo; kuimarisha viwanda vya nyama na maziwa na bidhaa zinazotokana na maziwa;

(v) Kuendeleza uvuvi, kuboresha zana za uvuvi na kuhakikisha upatikanaji wa vifaa bora vya kuhifadhi samaki;

(vi) Kutekeleza miradi muhimu ya miundombinu ikijumuisha reli, barabara, bandari, nishati na ujenzi wa Mkongo wa Taifa wa Mawasiliano. Miradi hii inajumuisha miradi ya kikanda ya Ukanda wa Kaskazini - Kusini unaounganisha ukanda wa shaba wa Zambia na DRC na Ukanda wa Kati (Dar es Salaam – Isaka – Rwanda – Burundi). Juhudi za kutafuta fedha kwa ajili ya kukamilisha upembuzi yakinifu zinaendelea. Aidha, mradi mwingine ni mradi wa umeme utakaounganisha Tanzania, Kenya na Zambia. Fedha kwa ajili ya utekelezaji wa mradi huu zinatafutwa;

(vii) Kuchukua hatua za kuimarisha mashirika ya umma kama vile ATCL, TRL, TPA kwa lengo la kuboresha huduma zinazotolewa na mashirika hayo;

(viii) Kuendelea kuboresha mazingira ya ukuaji wa sekta binafsi ikiwa ni pamoja na kuimarisha na kuendeleza ubia kati ya sekta ya umma na binafsi (PPP) hasa katika maeneo ya miundombinu na utoaji huduma kama vile za afya, maji, na elimu. Sera ya PPP

inakamilishwa na Serikali mwishoni mwa mwaka huu wa fedha (2008/09);

(ix) Kuchukua hatua za kurahisisha taratibu za kuwekeza na kufanya biashara nchini ili kuwapunguzia urasimu wawekezaji wa ndani na nje;

(x) Kuendelea kulinda mafanikio yaliyopatikana katika sekta za kijamii na kuboresha utoaji huduma, ikiwa ni pamoja na kuimarisha na kuboresha shughuli za ukaguzi na usimamizi wa elimu na kuboresha utoaji wa huduma za afya; na

(xi) Kuboresha sekta ya utalii kwa kuhamasisha utalii wa ndani, kutangaza vivutio vya utalii wetu nje; na kutafuta masoko hususan nchi za Asia.

**Malengo ya Uchumi Jumla na Maendeleo ya Jamii katika kipindi cha mwaka 2009/10 – 2011/12**

101. **Mheshimiwa Spika,** kutokana na msukosuko katika masoko ya fedha na mitaji na athari zake katika uchumi duniani, uchumi wa Tanzania nao umeanza kuathirika, hususan katika maeneo muhimu ya kilimo, utalii,

madini, na uwekezaji. Athari za msukosuko huu zinatarajiwa kuwa za mpito, na hivyo uchumi wetu unatarajiwa kuimarika tena katika kipindi cha muda wa kati. Kwa kuzingatia hayo, malengo ya sera za uchumi jumla katika mwaka 2009/10 -2011/12, yatakuwa yafuatayo:

(i) Pato Halisi la Taifa litakua kwa asilimia 5.0 mwaka 2009, asilimia 5.7 mwaka 2010 na kuongezeka hadi kufikia asilimia 7.2 mwaka 2011 na asilimia 7.5 mwaka 2012;

(ii) Kasi ya upandaji bei itapungua na kufikia chini ya asilimia 10 mwishoni mwa Juni 2010;

(iii) Mapato ya ndani yataongezeka kufikia uwiano na Pato la Taifa wa asilimia 15.9 mwaka 2008/09; asilimia 16.4 mwaka 2009/10; asilimia 17.2 mwaka 2010/11; na asilimia 18.3 mwaka 2011/12;

(iv) Kudhibiti ongezeko la ujazi wa fedha kwa tafsiri pana (M2) katika wigo utakaowiana na malengo ya ukuaji wa uchumi, na kasi ya upandaji bei na kuwa na akiba ya fedha za kigeni itakayoweza kukidhi mahitaji ya uagizaji wa bidhaa na huduma toka nje kwa kipindi kisichopungua miezi mitano;

(v) Kuwa na kiwango cha ubadilishaji wa fedha kitakachotokana na mwenendo wa soko la fedha za nje kati ya mabenki (IFEM)[2]; na

(vi) Kuondoa vikwazo vya kimfumo na kimuundo katika sekta ya fedha, ili kurahisisha upatikanaji wa mikopo kwa sekta binafsi.

**MAJUMUISHO**

102. **Mheshimiwa Spika**, kushuka kwa ukuaji wa uchumi kufikia asilimia 5.0 mwaka 2009 kutokana na athari za msukosuko wa kiuchumi duniani ambao nimeeleza hapo awali, kutaathiri malengo tuliyokuwa tumejiwekea ya ukuaji wa uchumi na kupunguza umaskini. Hivyo, ili kujinasua katika hali hiyo, tunalazimika kuchukua hatua za ziada, hususan katika sekta za kilimo na miundombinu ambayo ndiyo maeneo yatakayoweza kuchochea ukuaji wa uchumi kwa haraka na hivyo kuturudisha katika malengo yetu ya awali.

103. **Mheshimiwa Spika**, baada ya kueleza hali ya uchumi wa Taifa, matarajio, misingi na malengo ya mpango na bajeti kwa kipindi cha 2009/10 – 2011/12, napenda kusisitiza mambo muhimu ambayo tunahitaji

---
[2] *Inter-bank Foreign Exchange Market*

kuyapa kipaumbele katika utekelezaji na ufuatiliaji wa karibu kwa mwaka 2009/10 kama ifuatavyo:

(i) Kukabiliana na athari zinazotokana na msukosuko wa uchumi duniani;

(ii) Kuongeza uwekezaji katika maeneo yenye mwingiliano kisekta, hususan kilimo, miundombinu, uzalishaji viwandani na nishati, na kuhimiza ushiriki wa sekta binafsi katika maeneo hayo;

(iii) Kuongeza upatikanaji wa mikopo hasa kwa sekta ya kilimo kwa kuanzisha benki ya kilimo na ya wanawake;

(iv) Kuongeza uzalishaji wa mazao ya chakula;

(v) Kuongeza na kuboresha mapato ya ndani ili kuweza kugharamia sehemu kubwa ya matumizi ya Serikali na kuimarisha usimamizi katika matumizi ya fedha za umma;

(vi) Kuboresha mipango ya Uwezeshaji wa Wananchi Kiuchumi na Kuongeza Ajira; na

(vii) Kukamilisha upimaji wa ardhi ya vijiji.

104. **Mheshimiwa Spika,** napenda kueleza kuwa Tanzania inazo rasilimali nyingi ambazo kama tukiweza kuzitumia ipasavyo zinaweza kutusaidia kuondoa matatizo mengi ya kiuchumi na kijamii yanayotukabili. Kwa hiyo, unahitajika umakini zaidi katika matumizi ya rasilimali tulizonazo ili kuweza kuleta mabadiliko ya kiuchumi na kijamii kwa haraka zaidi. Kilimo Kwanza ndio kauli mbiu ya Serikali kwa mwaka 2009/10 kama nilivyosema hapo awali. Tunatarajia kuimarisha Benki ya Rasilimali na kufungua dirisha la mikopo ya kilimo katika benki hiyo na hatimaye kuanzisha Benki ya Kilimo; na kuhakikisha upatikanaji wa mikopo yenye masharti nafuu, na zana na pembejeo za kilimo kwa wakati kama Mheshimiwa Rais Jakaya Mrisho Kikwete, alivyosema jana. Vile vile hatua zitachukuliwa kunusuru maeneo yaliyoathirika na msukosuko wa kiuchumi hususan katika mazao, utalii na mabenki. Kadhalika, Serikali itaendelea na jukumu la kuwawezesha na kuunga mkono juhudi za wananchi kwa kuelekeza rasilimali tulizo nazo ili tuwe na maendeleo yenye kuwiana katika kila ngazi.

105. **Mheshimiwa Spika,** naomba kutoa hoja.

**Jedwali Na. 1: Ukuaji wa Pato la Taifa (GDP) kwa Shughuli za Kiuchumi kwa Gharama Zake (kwa bei za mwaka 2001)**

| SHUGHULI ZA KIUCHUMI | 2002 | 2003 | 2004 | 2005 | 2006 | 2007 | 2008 |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| **Kilimo, Uwindaji na Misitu** | **4.9** | **3.1** | **5.9** | **4.3** | **3.8** | **4.0** | 4.6 |
| Mazao | 5.6 | 3.2 | 6.6 | 4.4 | 4.0 | 4.5 | 5.1 |
| Mifugo | 2.8 | 2.2 | 4.1 | 4.4 | 2.4 | 2.4 | 2.6 |
| Uwindaji na Misitu | 3.3 | 3.0 | 2.7 | 3.6 | 4.6 | 2.9 | 3.4 |
| **Uvuvi** | **6.8** | **6.0** | **6.7** | **6.0** | **5.0** | **4.5** | 5.0 |
| **Viwanda na Ujenzi** | **9.4** | **10.9** | **10.9** | **10.4** | **8.5** | **9.5** | 8.6 |
| Uchimbaji Madini na Mawe | 16.9 | 17.1 | 16.0 | 16.1 | 15.6 | 10.7 | 2.5 |
| Bidhaa za Viwandani | 7.5 | 9.0 | 9.4 | 9.6 | 8.5 | 8.7 | 9.9 |
| Umeme na Gesi | 6.2 | 7.2 | 7.5 | 9.4 | -1.9 | 10.9 | 5.4 |
| Maji | 2.8 | 4.5 | 5.2 | 4.3 | 6.2 | 6.5 | 6.6 |
| Ujenzi | 11.9 | 13.8 | 13.0 | 10.1 | 9.5 | 9.7 | 10.5 |
| **Huduma** | **7.7** | **7.8** | **7.8** | **8.0** | **7.8** | **8.1** | 8.5 |
| Uuzaji Jumla, Rejareja na Matengenezo | 8.3 | 9.7 | 5.8 | 6.7 | 9.5 | 9.8 | 10.0 |
| Mahoteli | 6.4 | 3.2 | 3.6 | 5.6 | 4.3 | 4.4 | 4.5 |
| Uchukuzi | 5.9 | 5.0 | 8.6 | 6.7 | 5.3 | 6.5 | 6.9 |
| Mawasiliano | 10.4 | 15.6 | 17.4 | 18.8 | 19.2 | 20.1 | 20.5 |
| Fedha | 10.1 | 10.7 | 8.3 | 10.8 | 11.4 | 10.2 | 11.9 |
| Upangishaji Majengo na Huduma za Biashara | 7.1 | 6.5 | 6.8 | 7.5 | 7.3 | 7.0 | 7.1 |
| Utawala | 9.2 | 9.6 | 13.6 | 11.4 | 6.5 | 6.7 | 7.0 |
| Elimu | 7.0 | 2.8 | 4.0 | 4.0 | 5.0 | 5.5 | 6.9 |
| Afya | 8.6 | 8.7 | 7.8 | 8.1 | 8.5 | 8.8 | 9.0 |
| Huduma nyinginezo | 2.1 | 2.0 | 3.0 | 2.6 | 3.7 | 3.2 | 3.1 |
| Jumla ya Ongezeko la Thamani kabla ya Marekebisho | 7.2 | 6.9 | 7.8 | 7.4 | 6.8 | 7.3 | **7.5** |
| Toa Ushuru wa Huduma za Mabenki | 8.7 | 11.7 | 10.1 | 11.8 | 14.9 | 15.3 | 11.0 |
| Jumla ya Ongezeko la Thamani kwa Bei za Mwaka 2001 | 7.2 | 6.9 | 7.8 | 7.4 | 6.7 | 7.2 | **7.4** |
| Ongeza Kodi Katika Bidhaa | 7.2 | 6.9 | 7.8 | 7.4 | 6.8 | 6.9 | 7.8 |
| **Jumla ya Pato la Taifa (GDP $_{mp}$)** | **7.2** | **6.9** | **7.8** | **7.4** | **6.7** | **7.1** | **7.4** |

**Chanzo:** Ofisi ya Taifa ya Takwimu


**Jedwali Na. 2: Mchango wa Shughuli za Kiuchumi kwa Pato la Taifa kwa Gharama Zake (Kwa Bei za Miaka Husika)**

| SHUGHULI ZA KIUCHUMI | 2002 | 2003 | 2004 | 2005 | 2006 | 2007 | 2008 |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| **Kilimo, Uwindaji na Misitu** | **28.6** | **28.7** | **29.5** | **27.6** | **26.2** | **25.8** | **25.7** |
| Mazao | 21.4 | 21.8 | 22.4 | 20.5 | 19.2 | 19.0 | **19.0** |
| Mifugo | 4.8 | 4.7 | 4.8 | 5.0 | 4.8 | 4.7 | **4.7** |
| Uwindaji na Misitu | 2.4 | 2.3 | 2.3 | 2.2 | 2.2 | 2.1 | **2.0** |
| **Uvuvi** | **1.7** | **1.6** | **1.5** | **1.4** | **1.3** | **1.3** | **1.2** |
| **Viwanda na Ujenzi** | **19.6** | **21.0** | **20.8** | **20.8** | **20.8** | **21.2** | **21.0** |
| Uchimbaji Madini na Mawe | 2.1 | 2.4 | 2.6 | 2.9 | 3.2 | 3.5 | **3.4** |
| Bidhaa za Viwandani | 8.3 | 8.3 | 8.1 | 7.9 | 7.8 | 7.8 | **7.8** |
| Umeme na Gesi | 2.0 | 1.9 | 1.8 | 1.7 | 1.5 | 1.6 | **1.7** |
| Maji | 0.5 | 0.4 | 0.4 | 0.4 | 0.4 | 0.4 | **0.4** |
| Ujenzi | 6.8 | 8.0 | 7.9 | 7.8 | 7.8 | 7.8 | **7.7** |
| **Huduma** | **44.2** | **42.7** | **42.0** | **42.5** | **43.3** | **43.3** | **43.7** |
| Uuzaji Jumla, Rejareja na Matengenezo | 12.4 | 12.0 | 11.4 | 11.0 | 11.4 | 11.5 | **11.6** |
| Mahoteli | 2.6 | 2.4 | 2.3 | 2.5 | 2.6 | 2.7 | **2.6** |
| Uchukuzi | 5.0 | 4.8 | 4.6 | 4.4 | 4.3 | 4.2 | **4.2** |
| Mawasiliano | 1.2 | 1.3 | 1.5 | 1.7 | 2.1 | 2.3 | **2.5** |
| Fedha | 1.7 | 1.7 | 1.6 | 1.7 | 1.7 | 1.6 | **1.6** |
| Upangishaji Majengo na Huduma za Biashara | 9.7 | 9.4 | 9.1 | 9.5 | 9.6 | 9.5 | **9.6** |
| Utawala | 7.2 | 7.2 | 7.7 | 8.0 | 8.0 | 7.9 | **8.2** |
| Elimu | 2.0 | 1.8 | 1.7 | 1.6 | 1.5 | 1.4 | **1.3** |
| Afya | 1.5 | 1.4 | 1.4 | 1.5 | 1.5 | 1.6 | **1.5** |
| Huduma nyinginezo | 0.8 | 0.7 | 0.7 | 0.7 | 0.7 | 0.6 | **0.6** |
| Jumla ya Ongezeko la Thamani kabla ya Marekebisho | 94.1 | 94.0 | 93.7 | 92.3 | 91.7 | 91.6 | **91.6** |
| Toa Ushuru wa Huduma za Mabenki | -0.9 | -0.9 | -0.9 | -0.9 | -0.9 | -1.0 | **-1.1** |
| Jumla ya Ongezeko la Thamani kwa Bei za Mwaka 2001 | 93.3 | 93.1 | 92.8 | 91.4 | 90.7 | 90.7 | **90.6** |
| Ongeza Kodi Katika Bidhaa | 6.7 | 6.9 | 7.2 | 8.6 | 9.3 | 9.3 | **9.4** |
| **Jumla ya Pato la Taifa (GDP $_{mp}$)** | **100.0** | **100.0** | **100.0** | **100.0** | **100.0** | **100.0** | **100.0** |


**Chanzo:** Ofisi ya Taifa ya Takwimu

**Jedwali Na. 3: Pato la Taifa kwa Gharama Zake (Kwa Bei za Mwaka 2001)**


| Economic Activity | 2001 | 2002 | 2003 | 2004 | 2005 | 2006 | 2007r | 2008p |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| **Kilimo, Uwindaji na Misitu** | **2,636,193** | **2,766,479** | **2,850,956** | **3,017,988** | **3,148,384** | **3,268,238** | **3,399,648** | **3,554,488** |
| Mazao | 1,945,945 | 2,055,634 | 2,122,361 | 2,262,725 | 2,361,930 | 2,457,373 | 2,567,955 | 2,698,921 |
| Mifugo | 459,448 | 472,500 | 483,001 | 503,000 | 525,109 | 537,498 | 550,398 | 564,708 |
| Uwindaji na Misitu | 230,800 | 238,345 | 245,594 | 252,263 | 261,345 | 273,367 | 281,295 | 290,859 |
| **Uvuvi** | **153,660** | **164,049** | **173,892** | **185,543** | **196,676** | **206,510** | **215,734** | **226,521** |
| **Viwanda na Ujenzi** | **1,638,459** | **1,792,024** | **1,988,081** | **2,204,619** | **2,433,261** | **2,639,902** | **2,889,519** | **3,138,241** |
| Uchimbaji Madini na Mawe | 159,979 | 187,000 | 219,000 | 254,000 | 295,000 | 341,000 | 377,559 | 386,998 |
| Bidhaa za Viwandani | 762,400 | 819,200 | 893,000 | 977,000 | 1,071,000 | 1,162,000 | 1,263,435 | 1,388,515 |
| Umeme na Gesi | 196,860 | 209,000 | 223,953 | 240,708 | 263,218 | 258,347 | 286,507 | 301,978 |
| Maji | 43,840 | 45,084 | 47,128 | 49,557 | 51,700 | 54,905 | 58,474 | 62,333 |
| Ujenzi | 475,380 | 531,740 | 605,000 | 683,354 | 752,343 | 823,650 | 903,544 | 998,416 |
| **Huduma** | **4,139,962** | **4,460,699** | **4,806,587** | **5,182,094** | **5,596,784** | **6,035,932** | **6,527,561** | **7,085,136** |
| Uuzaji Jumla, Rejareja na Matengenezo | 1,182,797 | 1,281,544 | 1,405,698 | 1,486,931 | 1,585,906 | 1,736,631 | 1,906,821 | 2,097,503 |
| Mahoteli | 250,978 | 267,162 | 275,836 | 285,732 | 301,873 | 314,921 | 328,859 | 343,658 |
| Uchukuzi | 487,062 | 516,000 | 541,901 | 588,574 | 627,951 | 661,000 | 703,965 | 752,539 |
| Mawasiliano | 112,783 | 124,549 | 144,039 | 169,158 | 200,900 | 239,537 | 287,684 | 346,659 |
| Fedha | 140,000 | 154,108 | 170,643 | 184,775 | 204,694 | 228,000 | 251,280 | 281,120 |
| Upangishaji Majengo na Huduma za Biashara | 936,440 | 1,003,260 | 1,068,732 | 1,141,014 | 1,226,790 | 1,316,000 | 1,408,120 | 1,508,097 |
| Utawala | 640,649 | 699,561 | 766,760 | 871,169 | 970,786 | 1,033,488 | 1,102,951 | 1,180,158 |
| Elimu | 188,733 | 202,000 | 207,606 | 215,910 | 224,547 | 235,774 | 248,742 | 265,905 |
| Afya | 118,972 | 129,229 | 140,437 | 151,370 | 163,572 | 177,520 | 193,142 | 210,525 |
| Huduma nyinginezo | 81,548 | 83,286 | 84,935 | 87,461 | 89,765 | 93,061 | 95,998 | 98,974 |
| Jumla ya Ongezeko la Thamani kabla ya Marekebisho | **8,568,274** | **9,183,251** | **9,819,516** | **10,590,244** | **11,375,105** | **12,150,582** | **13,032,462** | **14,004,385** |
| Toa Ushuru wa Huduma za Mabenki | -80,000 | -87,000 | -97,154 | -106,931 | -119,497 | -137,287 | -158,292 | -175,704 |
| Jumla ya Ongezeko la Thamani kwa Bei za Mwaka 2001 | **8,488,274** | **9,096,251** | **9,722,362** | **10,483,313** | **11,255,608** | **12,013,295** | **12,874,170** | **13,828,681** |
| Ongeza Kodi Katika Bidhaa | 612,000 | 655,926 | 701,372 | 756,422 | 812,482 | 867,868 | 927,751 | 999,664 |
| **Jumla ya Pato la Taifa (GDP $_{mp}$)** | **9,100,274** | **9,752,177** | **10,423,734** | **11,239,735** | **12,068,090** | **12,881,163** | **13,801,921** | **14,828,345** |



Kielelezo Na. 1: Mwenendo wa Bei 2007 - 2008
20.0%
18.0%
16.0%
14.0%
12.0%
10.0%
8.0%
6.0%
4.0%
2.0%
0.0%
Chakula, 18.5%
Jumla, 13.5%
Zisizo za Chakula, 6.0%
Usafiri, 5.13%
Jan
Feb
Mac
Apr
Mai
Jun
Jul
Agos
Sep
Oct
Nov
Dec
2007
2008

**Kielelezo Na. 2: Mwenendo wa Viwango vya Ubadilishanaji wa Dola za Kimarekani**



**Kielelezo Na. 3: Mgawanyo wa Bidhaa Zilizouzwa Nje**



**Jedwali Na. 4: Thamani ya Ununuzi wa Bidhaa Nje (USDmillion)**

| Aina ya Bidhaa | 2002 | 2003 | 2004 | 2005 | 2006 | 2007 | 2008 P | 2007-2008 (Badiliko %) |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| **Bidhaa za Kukuza Mitaji** | **656.3** | **741.5** | **860.0** | **1,078.1** | **1,435.1** | **1,765.0** | **2,648.6** | **50.1%** |
| Vifaa vya Usafiri | 198.6 | 212.5 | 229.0 | 289.6 | 374.8 | 477.8 | 787.8 | 64.9% |
| Majengo na Ujenzi | 122.6 | 151.3 | 185.5 | 257.2 | 338.0 | 416.7 | 619.5 | 48.7% |
| Mitambo | 335.1 | 377.7 | 445.5 | 531.3 | 722.4 | 870.5 | 1,241.3 | 42.6% |
| **Bidhaa za Kati** | **384.9** | **618.4** | **856.0** | **1,166.3** | **1,576.9** | **1,970.7** | **2,514.9** | **27.6%** |
| Mafuta | 177.3 | 367.0 | 575.0 | 847.3 | 1,146.5 | 1,462.1 | 1,838.6 | 25.7% |
| Mbolea | 18.3 | 26.0 | 54.1 | 64.6 | 53.9 | 59.1 | 150.4 | 154.4% |
| Mali Ghafi za Viwanda | 189.3 | 225.4 | 227.0 | 254.4 | 376.5 | 449.4 | 525.9 | 17.0% |
| **Bidhaa za Matumizi ya Kawaida** | **467.9** | **571.4** | **764.7** | **751.0** | **849.9** | **1,122.7** | **1,274.2** | **13.5%** |
| Chakula | 134.0 | 166.0 | 248.8 | 168.4 | 249.2 | 315.4 | 290.9 | -7.8% |
| Bidhaa Nyinginezo | 333.9 | 405.4 | 515.9 | 582.6 | 600.7 | 807.3 | 983.4 | 21.8% |
| **Jumla Kuu (F.O.B)** | **1,511.3** | **1,933.5** | **2,482.8** | **2,997.6** | **3,864.1** | **4,860.6** | **6,439.9** | **32.5%** |
| **Jumla Kuu (C.I.F)** | **1,660.8** | **2,124.7** | **2,728.4** | **3,294.0** | **4,246.3** | **5,341.4** | **7,076.8** | **32.5%** |

**Chanzo**: *Benki Kuu ya Tanzania*

*P: Makadirio*

**Jedwali Na 5: Mizania ya Malipo na Nchi za Nje (USD Milioni)**

| | 2002r | 2003r | 2004r | 2005r | 2006r | 2007r | 2008p |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| Urari wa Biashara | (531.7) | (717.3) | (1,001.2) | (1,318.5) | (1,946.5) | (2,634.1) | **(3,403.2)** |
| Zilizouzwa Nje (fob) | 979.6 | 1,216.1 | 1,481.6 | 1,679.1 | 1,917.6 | 2,226.6 | **3,036.7** |
| Zilizonunuliwa toka Nje (fob) | 1,511.3 | 1,933.5 | 2,482.8 | 2,997.6 | 3,864.1 | 4,860.6 | **6,439.9** |
| Urari wa Huduma | 287.6 | 222.1 | 158.9 | 61.8 | 278.7 | 460.3 | **570.9** |
| Mapato | 920.1 | 947.8 | 1,133.6 | 1,269.2 | 1,528.1 | 1,875.7 | **2,168.9** |
| Malipo | 632.5 | 725.7 | 974.7 | 1,207.3 | 1,249.4 | 1,415.4 | **1,598.0** |
| Urari wa Mapato ya Vitega Uchumi | (88.8) | (149.1) | (112.4) | (102.0) | (64.1) | (58.1) | **(118.1)** |
| Yaliyoingia | 67.9 | 87.1 | 81.8 | 80.9 | 80.3 | 107.3 | **121.6** |
| Yaliyotoka | 156.8 | 236.2 | 194.2 | 182.9 | 144.4 | 165.4 | **239.7** |
| Urari wa Uhamisho Mali ya Kawaida | 416.6 | 556.9 | 588.8 | 495.7 | 588.7 | 651.5 | **617.0** |
| Iliyoingia | 477.9 | 619.9 | 653.8 | 563.3 | 654.6 | 724.0 | **697.2** |
| O/W Serikalini | 427.7 | 553.3 | 581.7 | 477.9 | 559.7 | 626.9 | **594.2** |
| Iliyotoka | 63.0 | 63.0 | 65.0 | 67.5 | 65.9 | 72.5 | **80.2** |
| Urari wa Biashara ya Bidhaa, Huduma na | 83.6 | (87.5) | (365.9) | (862.8) | (1,143.2) | (1,580.3) | **(2,333.4)** |
| Urari wa Uhamisho Mitaji | 785.7 | 692.8 | 459.9 | 393.2 | 5,183.5 | 923.7 | **637.5** |
| Iliyoingia | 785.7 | 692.8 | 459.9 | 393.2 | 5,183.5 | 923.7 | **637.5** |
| Iliyotoka | - | - | - | - | - | - | **-** |
| Urari Katika Uwekezaji | 255.4 | 61.2 | 306.3 | 555.6 | (3,954.6) | 946.0 | **1,883.3** |
| Uwekezaji Katika Maradi | 387.6 | 308.2 | 330.6 | 494.1 | 597.0 | 647.0 | **744.0** |
| Uwekezaji Katika Hisa | 2.2 | 2.7 | 2.4 | 2.5 | 2.6 | 2.8 | **2.9** |
| Uwekezaji Aina Nyingine | (134.4) | (249.7) | (26.7) | 59.0 | (4,554.2) | 296.3 | **1,136.4** |
| Makosa na Masahihisho | (806.8) | (277.4) | (116.3) | (313.7) | 375.0 | 123.3 | **(78.7)** |
| Urari wa Malipo Yote | 317.9 | 389.1 | 284.0 | (227.8) | 460.7 | 412.6 | **108.81** |

**Chanzo**: *Benki Kuu ya Tanzania*